ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 5 Februari, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Mwenyekiti, (Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa) Alisoma Dua

TAARIFA YA MHE. MWENYEKITI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaanza shughuli zetu kuna maelekezo hapa ambayo naomba kusoma ili tuelewane. Kwa kuwa tumekuwa na utaratibu wa Baraza la Wawakilishi kupokea wageni mbali mbali kwa lengo la kujionea shughuli za Baraza zinavyokwenda. Napenda kuwajulisha kuwa leo tarehe 05/02/2014 katika ukumbi huu kuna wanafunzi wa Skuli ya Sekondari ya Dole, idadi yao ni 40, wakiongozwa na mkuu wa msafara ambaye ni mwalimu Abass Mdungi Mohammed. Naomba asimame. *(Makofi).*

Pia, wamefuatana na Diwani wa Dole Mhe. Masoud Abraham Masoud. Naomba asimame. Aidha, wageni hawa wamekuja kwa niaba ya Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Dole Mhe. Shawana Bukheit Hassan. Kwa heshima naomba tutambuwe kuwepo kwao. Naomba msimame ili muonekane wote kwa jumla. *(Makofi).*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 50

Kupongezwa kwa Vikosi vya Serikali kwa Gwaride la Sherehe za Mapinduzi

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa kusherehekea miaka 50 (nusu karne) ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa kuwa miongoni mwa mapambo ya sherehe ni kuliona Jeshi la nchi likipita kwa ukakamavu mbele ya Mhe. Rais na mbele ya wananchi na kwa kuwa Zanzibar ni nchi na ina vikosi mbali mbali vya Jeshi kama vile JKU, KMKM, KVZ, na KZU.

(a) Je, ni mara ngapi tokea viundwe vikosi hivyo vimepongezwa kwa gwaride lililopamba sherehe za Mapinduzi.

(b)Kama bado ni sababu zipi za msingi zinazopelekea kutokupongezwa kwa vikosi vyetu kwa gwaride la sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia salama na kuturudisha tena katika Baraza hili ili tuweze kuendelea na shughuli zetu. Aidha, na mimi nichukuwe fursa hii Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze vijana wetu waliokuja kututembelea. Pia, nimpongeze na mwakilishi wao kwa kutengeneza utaratibu huu wa vijana hawa kuja ili wapate nafasi ya kujifunza vizuri shughuli za Baraza ili hapo baadae tupate wawakilishi wazuri wa Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 50 lenye vifungu (a) na (b), kwa ruhusa yako naomba kwanza nipokee pongezi alizotoa Mhe. Mwakilishi, kwa maadhimisho ya sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, naomba kutanguliza maelezo yafuatayo;

Mhe. Mwenyekiti, Sherehe za Mapinduzi zinaratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa usimamizi wa Halmashauri ya sherehe na maadhimisho ya kitaifa ambayo mwenyekiti wake ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzinar.

Halmashauri hii inazo kamati 9 na sekreterieti moja na zinatekeleza majukumu yake mbali mbali kama inavyoelekezwa na Halmashauri hiyo. Miongoni mwa kamati hizo ni kamati ya gwaride.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 50 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kawaida ifikapo tarehe 12 Januari ya kila mwaka katika kilele cha maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hutoa shukrani na pongezi maalum, kwa vikosi vya ulinzi na usalama kwa gwaride zuri wanalolionesha na ukakamavu wao na pia kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao. Pamoja na pongezi hizo Mhe. Rais, pia, hutoa pongezi kwa waandaaji wa sherehe hizo ambao ni Halmashauri ya Sherehe na

Maadhimisho ya Kitaifa, pamoja na kamati zake zikiwemo kamati za gwaride.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba serikali itaendelea kuwashukuru na kuwapongeza askari wetu na wale wote ambao wanatoa michango yao katika kufanikisha sherehe hizi na wananchi mbali mbali kwa ajili ya kutimiza sherehe zetu za Mapinduzi na sherehe nyengine za kitaifa.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, napenda kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ina sherehekea Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar kila mwaka na kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina idara maalum za SMZ, ambapo ni vikosi vilivyopo Zanzibar. Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba sherehe zote zinaratibiwa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

(a)Je, ni mara ngapi vikosi vya SMZ vimeweza kuliongoza gwaride la sherehe ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(b)Kwa kuwa kunakuwa na Sherehe za Muungano, ni mara ngapi vikosi vya SMZ vimeshiriki kigwaride katika Sherehe za Muungano.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni utaratibu tu uliowekwa wa kijeshi, kwamba wanaongoza gwaride pale huwa ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Napenda ieleweke kwamba jeshi lile ni la Muungano na maana ya Muungano ni nchi mbili huru zilizoungana. Kwa hivyo, pia lile ni jeshi letu na ni utaratibu wa kawaida, vikosi ni vyetu na lile ni jeshi letu. Kwa hivyo, ni uwamuzi tu kwamba Jeshi la Wananchi liongoze gwaride lile, liongoze na vikosi vyetu vyengine ni utaratibu tu wa kawaida, sio kwamba yuko mmoja mkubwa na mmoja mdogo, hapana. Ni utaratibu tu wa kawaida wa Kijeshi wanaofanya wenyewe. Napenda tukubali kwamba Jeshi letu la Wananchi linafanya kazi nzuri ya kulinda mipaka yetu ikiwemo na mipaka ya Zanzibar.

Vile vile, kuna swali liliulizwa kwa nini vikosi vya SMZ havishiriki katika Sherehe za Muungano kule Tanzania Bara. Nafikiri ushauri wako ni mzuri Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, tutaangalia suala hili ili tuone ni namna gani na vikosi vyetu ya SMZ vipate nafasi ya kushiriki. Ni utaratibu wa gharama tu, katika kupunguza gharama ndio maana tunashirikisha vikosi vile vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini hakuna tatizo lolote kwa nini vikosi vya SMZ visishiriki kule. Tutakapokuwa na fedha za kutosha za

kufanya hivyo, basi tunaweza kuamua ni maamuzi tu, wala hakuna tatizo la aina yoyote ile. Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Moja katika sherehe zetu za Mapinduzi zilizofanyika za miaka 50, tulishuhudia katika Uwanja wetu wa Aman zikipita silaha mbali mbali za nchi yetu, katika kuonesha ukakamavu na kuonesha wananchi silaha zetu zilizopo. Lakini tu baada ya sherehe zana zile zilipakiwa katika meli zikarudi Tanzania Bara.

Je, Zanzibar hatuna sehemu za kuhifadhia zana zile au ni kwa sababu ipi zana zile kuhamishwa zikenda Tanzania Bara.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema majeshi yana utaratibu wao na yana maeneo yao ya kuweka silaha fulani fulani. Baadhi ya silaha ziko hapa Zanzibar na zipo za kutosha. Kwa hivyo, nataka niwaambie tu kwamba maadui wanaoitizama Zanzibar kwa jicho la husuda, wasije kufanya mchezo vitu vipo. Kwenye zile Sherehe za Mapinduzi tulionesha tu rambirambi za uwezo wa jeshi letu.

Kwa hivyo, tunavyo vitu vipo na vinawekwa hapa Zanzibar na kwa sababu ya Sherehe ilitubidi kuleta vitu vyengine kutoka Tanzania Bara. Kama nilivyosema hili ni jeshi letu na uwamuzi ni wetu, tunavyoamua basi tunafanya hivyo na tukitaka kujenga maghala mengine ya silaha hapa tutajenga ni uamuzi wetu tu.Kwa hvyo, sio tatizo hilo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na vikosi hivyo kupongezwa, lakini vikosi hivyo huanza mazoezi takriban kwa muda wa mwezi mmoja kabla ya sherehe.

Je, Mhe. Waziri, baada ya kumalizika kwa sherehe hizo, vikosi hivi vimepangiwa siku za mapumziko ili waweze kupumzika baada ya sherehe zile. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hasa maaskari wana utaratibu wao na mara nyingi wanafanya mambo yao kwa siri wanazozijua wao. Mara nyingi kama raia kuna mambo mengine huwa hawatuambii. Kwa hivyo, wana utaratibu wao ambao wanaufanya wa mapumziko na kufanya shughuli zao wanavyojua wao wenyewe, huwa hawatuambii sisi kuwa wanafanya nini, lakini naamini kabisa

baada ya kazi nzuri ile huwa wanatengeneza utaratibu mzuri wa mapumziko na wakati huo huo wengine wanalinda nchi yetu.

Nam. 17

Mabadiliko ya Maeneo ya Michango Katika Mfuko wa Jimbo

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Kuna taarifa kuwa katika semina iliyofanyika kwa ajili ya Makatibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Baraza la Wawakilishi kumetokea mabadiliko katika maeneo ya kupeleka michango hiyo ya Mfuko kwa jamii.

(a) Taarifa hiyo ni ya kweli.

(b) Ni maeneo gani yameongezeka kutoa misaada.

(c) Ni maeneo gani ambayo zamani yalikuwamo na kuondolewa baada ya semina hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, haina taarifa ya mabadiliko ya kupeleka michango ya Mfuko wa Jimbo katika baadhi ya maeneo ya majimbo kinyume na utaratibu wa sheria ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilifanya mafunzo kwa Makatibu wa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, kwa Maafisa Mipango wa Wilaya na Waratibu wa Wilaya na Mikoa wa Kisiwani Pemba. Dhamira kubwa ya mafunzo hayo ilikuwa ni kuwafahamisha wadau kuhusu maudhui ya sheria nambari 4 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2012, kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wake. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pia ina dhamira ya kufanya semina kama hiyo kwa upande wa Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu na Waheshimiwa Wajumbe, waelewe kwamba katika semina hiyo washiriki walifafanuliwa vipengele mbali mbali vilivyomo ndani ya sheria hiyo na sio kuifanyia mabadiliko au kubadilisha maamuzi ya miradi ya Kamati za

Maendeleo za Majimbo. Kwani ni Baraza lako tukufu kwa mujibu wa katiba ndio lenye uwezo wa kufanya marekebisho ya sheria na si vyenginevyo. Fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya Maendeleo ya Jimbo, zinatakiwa kutumika kwa mujibu wa sheria iliopo.Hivyo, hakuna mtu au kikundi cha watu wenye uwezo wa kufanya kinyume na utaratibu huo wa sheria.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja la nyongeza, baada ya kupata majibu ya kuridhisha kutoka kwa Mhe. Waziri kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, katika kikao cha hivi karibuni nilichokifanya katika jimbo langu pamoja na kamati yangu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, kulikuwa na kazi kubwa ya kutofahamiana kwa baadhi ya miradi.

Kwa mfano sheria haikueleza kuwa tusaidie katika kujenga Misikiti, vyuo na kadhalika. Lakini tulipozungumza hapa tukapitisha kwa umoja wetu, tena tukakubaliwa kufanya hivyo. Sheria haikueleza kuwa vikundi vya watu waliojikusanya wakawa na shughuli zao wakulima wasisaidiwe chochote, wala sheria haikueleza kuwa sisi Mfuko wetu wa Jimbo ushughulikie kwenye ile miradi ambayo ni mikubwa tu. Kama shule, barabara au maji na kadhalika.

Sasa katika kufanya kikao hiki, katibu wangu ambaye alihudhuria katika kikao hicho na tena ni makini sana na ana uwezo, basi alieleza wazi kuwa kuna mambo yalikatwa na akasema hata hii habari ya dini. Kweli wawakilishi walijitahidi sana kutetea, lakini sisi tunayakata na mambo haya yasifanywe tena. Sasa ikiwa Mhe. Waziri anasema hivyo, lakini watendaji wake wa semina ndio walivyoelekeza.

Je, haoni kuwa ipo haja ya kuwafahamisha watu wake, kuwa hakuna mtu yeyote anayeweza kubadilisha kitu ambacho sisi tumeshakipitisha hapa, ili tusiwe na migogoro baina yetu sisi na watendaji wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, swali hili la Mhe. Mjumbe lilikuwa na maelezo marefu, ambapo mara nyengine anaweza kukutoa kwenye mstari, halafu akakurudisha tena kwenye mstari. Lakini nia ni kwamba yeye na sisi hapa tunasisitiza kwamba Sheria ya Mfuko wa Jimbo iheshimiwe, taratibu zake zifuatwe na kusikiukwe utaratibu uliowekwa. Taratibu za Mfuko wa Jimbo ndio zifanye kazi, hakuna mtu mwenye uwezo wa kubadilisha maamuzi yale ya sheria. Hata sisi wenyewe wawakilishi, hatuwezi kufanya mabadiliko bila ya kuleta hapa kwa kufuata utaratibu wa kufanya mabadiliko ya sheria ndani ya Baraza hili.

Kwa hivyo, napenda sheria tunazozitunga tuziheshimu, tuzitekeleze na tuzifuate. Kama kuna kipengele kinachoruhusu kufanya utaratibu kama

alioueleza Mhe. Salim Abdalla Hamad, basi tufanye hivyo. Kama hakipo basi tuheshimu maamuzi ambayo tumeyafanya.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametuwezesha kufika katika Baraza lako tukufu kwa hali ya afya njema na usalama.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mfuko huu wa majimbo ni mfuko wa kusaidia wananchi na kwa kuwa wanawake wa nchi hii na wao huwa wanasaidia na wanawake wana kazi kubwa zaidi ya kuwasaidia wanawake wenzao.

(a) Je, ni lini na akinamama na wao watapatiwa japo nusu ya mfuko huu, ili kusaidiana katika majimbo na mikoa.

(b) Kwa kuwa Waheshimiwa Wawakilishi wenyewe ndio waliyoiomba serikali kupata mfuko wa jimbo na kwa kuwa serikali hii hii ilikubali kutoa fedha za mfuko wa jimbo. Je, mahesabu ya mfuko huu wa jimbo yanakwendaje.

(c) Mhe. Mwenyekiti, halafu kuna maelezo ambayo sio ya kuaminika kwamba Waheshimiwa Wawakilishi baadhi yao pesa hizi hazifiki majimboni. Je, kama hazifiki majimboni wanachukuliwa hatua gani za kisheria na wakati tumepitisha sisi humu katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wenye uwezo wa maamuzi ya kisheria ni Baraza lako tukufu na kwa kuwa hivi sasa tumo katika mchakato wa mwisho wa kutengeneza sheria ya utawala wa Baraza, ambapo pamoja na mambo mengine yatahusiana pia na suala zima la mambo haya ya masurufu na maendeleo katika majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Asha Bakari Makame, tusubiri utaratibu wa sheria itakapokuja, ili sisi wenyewe tutakapoijadili basi tuweke hivyo vipengele tunavyoona vinafaa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu.

Aidha, kuhusu mahesabu. Sheria ile imeweka wazi kabisa kuhusu utaratibu wa matumizi ya fedha za maendeleo ya mfuko wa jimbo. Kwa wale ambao hawafuati utaratibu, basi sheria itawakalia kifuani. Kwa hivyo, nawaomba sana waheshimiwa tutekeleze wajibu huo, kwa sababu hivi sasa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, inapita katika majimbo kuratibu ili kuona namna ya utekelezaji wa fedha zilizotolewa katika majimbo. Vyenginevyo inaweza kuwa muhadhara kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Nam. 28

Sababu ya Wafanyakazi Kutorekebishiwa Mishahara Kwa Wakati Baada ya Mafunzo

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Mafao ya wafanyakazi hupanda na kuongezeka kutokana na aidha kipindi kirefu cha utumishi, ongezeko la taaluma kwa watumishi au kupandishwa kwa mishahara ya watumishi wa umma na Mkuu wa Nchi (Rais). Kwa kuwa watumishi katika Wizara mbali mbali huomba nafasi ya kusoma ili kuongeza taaluma pamoja na ujuzi katika utumishi wao na hatimae hurejea maofisini mwao kwa ajili ya kuendelea na ajira pale wanapomaliza aidha Cheti, Stashahada, Shahada pamoja na Shahada za uzamili pamoja na uzamivu.

Je, ni sababu gani za msingi zinazoifanya wizara yako ishindwe au kuchelewa kuwarekebishia mishahara yao watumishi wa umma pale wanapomaliza mafunzo yao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma) – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 28, kuna maelezo kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma ndio ofisi inayoshughulikia maslahi ya watumishi, kwa mujibu wa kifungu 49 cha Sheria ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar namba 2 ya mwaka 2011. Kiutaratibu mtumishi wa umma anaporudi masomoni Wizara/Taasisi husika huwasilisha Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma, barua iliyoambatanishwa na vivuli vya vyeti vya kumalizia masomo, tarehe ya ajira, namba ya ajira pamoja na mshahara anaopokea mtumishi huyo kabla hajaenda masomoni. Baada ya kuwasilishwa taarifa hizo za mtumishi katika ofisi hii na kuhakikiwa ipasavyo, ofisi hii humwandikia Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, kwa ajili ya kufanyia marekebisho ya mshahara wa mtumishi huyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 28 kama ifuatavyo:-

Kuchelewa kufanyiwa marekebisho ya mshahara kwa watumishi wa umma anaporejea kutoka masomoni, kunaweza kutokea kutokana na sababu zifuatazo:-

Sababu ya Kwanza: Ili mtumishi wa umma aweze kufanyiwa marekebisho ya mshahara anapaswa kuwasilisha nakla ya cheti cha kumalizia masomo, lakini mara nyingi watumishi huwasilisha '*Statement of Result*' au '*Privisonal Result'* na kudai kufanyiwa marekebisho ya mshahara jambo ambalo ni kinyume na taratibu za kiutumishi.

Sababu ya Pili: Baadhi ya wakati taarifa za mtumishi zinazotumwa huwa hazikamiliki; kwa mfano kutokuwepo au kusahauliwa kuambatanishwa kwa vivuli vya vyeti, taarifa za tarehe ya ajira, nambari ya ajira na mshahara anaolipwa mtumishi hivi sasa. Hali hii hupelekea ofisi hii kuitaka tena taasisi husika kukamilisha taarifa hizo za mtumishi ili kukamilisha taratibu za kumrekebishia mshahara wake.

Sababu ya Tatu: Maslahi ya watumishi wa umma, hushughulikiwa na taasisi zaidi ya moja; Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma na Wizara ya Fedha. Utaratibu ambao unaweza kuchangia ucheleweshaji wa marekebisho ya mshahara. Kama nilivyofafanua katika maelezo yangu ya awali kuwa, baada ya kupokea barua ya marekebisho ya mshahara na kufanyiwa uhakika, ndipo inapowasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho ya mshahara katika '*Payroll'*. Wizara ya Fedha ndiyo inayosimamia marekebisho hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hii, mazungumzo yanaendelea kuhakikisha kuwa suala hili linashughulikiwa na wizara moja, inayoshuhulikia maslahi ya watumishi ili kuondosha malalamiko mbali mbali yanayojitokeza, ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji wa marekebisho ya mishahara ya watumishi wa umma.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ambaye kwa sasa ni Kaimu Waziri katika masuala ya madughuli. Naomba niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti, mpaka hivi sasa nauliza swali hili kuna watumishi kadhaa ambao tayari wamemaliza masomo yao katika vyuo vikuu kadhaa hapa nchini, na kwa kuwa ushahidi upo kwani kuna kijana anayeitwa Ali Ali Khamis, huyu ni mtumishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, ambaye yuko katika kitengo cha uhasibu na ndiye mshika fedha wa wizara kule Pemba. Amemaliza masomo yake karibu mwaka huu. Wachilia mbali kuwasilisha vivuli, yeye amewasilisha vyeti vyenyewe vya *Master Degree in Accountant*, amewasilisha cheti chenyewe.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hii kesi sasa hivi huu ni mwaka na hii kesi imeshafika mpaka kwa Mhe. Waziri na hadi leo hii marekebisho hayo Mhe. Mwenyekiti hayajafanywa. Je, hii ni roho mbaya, husuda au ni uadui wa watumishi kwa watendaji katika ofisi hii ya masuala ya utumishi.

(b) Kuchelewa na kutofanyiwa marekebisho hawa watumishi ambao wamesota sana katika vyuo vikuu kupata elimu na kwamba mpaka hii leo hawajafanyiwa madughuli yao. Hii ni kwa sababu serikali haiwajali watumishi wake au vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma): Mhe. Mwenyekiti, nia ya serikali siku zote ni kuhakikisha kwamba watumishi wetu wanapewa huduma vizuri, wanapewa mishahara yao kwa wakati na serikali isingependa kabisa kumnyanyasa ama kumsumbua mtumishi yeyote wa umma. Ndio maana serikali ikaweka utaratibu wa makusudi wa kupandisha mishahara na kutoa vivutio vyengine kwa ajili ya kuwavutia wafanyakazi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, linapotokea tatizo basi mara nyingi inakuwa ni makosa ya kibinadamu. Namuomba Mhe. Saleh Nassor Juma, uniwachie suala hili la Ndugu Ali Ali Khamis, ili tulifuatilie na tuone ukweli wake na pia, tuyapeleke maelezo haya kwamba watumishi wengi bado wapo kadhaa hawajapata majibu sahihi kuhusu mishahara yao ili jambo hili lifatiliwe na kama lipo basi lipate majibu sahihi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii. Naomba nimuulize Mhe. Waziri, kwamba katika suala la marekebisho ya mishahara kwa miaka kadha sasa tumekuwa tukipitisha bajeti au fungu la bajeti kwa ajili ya kufanyia kazi hiyo. Na katika mwaka huu wa fedha unaonendelea Baraza hili lilipitisha takriban bilioni 17.5 kwa ajili ya kufanya marekebisho hayo. Lakini kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi, kwamba waliofaidika kwa miaka yote hiyo wameendelea kuwa ni wafanyakazi wa kada za juu na wale walioitwa wataalam.

Lakini wafanyakazi wengi watumishi wa umma ambao ndio wanaowapa *support* na kupelekea hao wataalam kufanya kazi zao, marekebisho hayo yaliyofanyika wengi wamepewa kiwango kinacholingana cha 25,000 ndio nyongeza yao wakati kuna tofauti kubwa sana na wengine wameongezewa kwa kima kikubwa sana. Je, hatuoni kwamba serikali kwa kufanya hivi itapelekea kuzorota kwa kazi, kwa sababu inawavunja moyo wafanyakazi wa chini pamoja na kuwa na lengo zuri la kusaidia wataalam, lakini haioni kwamba mpishano baina ya mishahara haupaswi kuwa mkubwa sana kiasi cha kuleta hali ya matabaka ndani ya watumishi wa umma.

Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti ni kweli kuwa upo umuhimu kabisa kabisa kuangalia maslahi ya wafanyakazi wetu hususan wale wafanyakazi wenye uzoefu kwa sababu wafanyakazi wenye taaluma mbali mbali utaratibu umewekwa vizuri na mishahara yao inakwenda vizuri. Lakini naamini na upo mchakato hasa wa makusudi wa kulifanya zoezi hili ili kuondosha haya malalamiko na kasoro zinazojitokeza hasa hasa kwenye wafanyakazi wazoeefu.

Hili jambo limezungumzwa sana na naamini sasa hivi liko katika hatua nzuri ya kupata ufumbuzi wa tatizo hilo. Namuomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Waheshimiwa Wajumbe wavute subira wakati serikali wanashughulikia jambo hili ili tupate ufumbuzi ulio sahihi katika kutatua tatizo hili na wafanyakazi wote waweze kupata stahiki yao vizuri washerehekee na wafurahie matunda ya kufanya shughuli zao vizuri.

Nam. 25

Kuharibika kwa Kidaraja cha Gombani Mpya

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Wananchi wa Ng'ambwa Gombani ya Kati, Simwambili na Gawani huunganisha barabara kuu iendayo Chake/Wete kupitia kwenye kidaraja kidogo kinachopandia uwanja wa Gombani (mpya) na kwa kuwa kidaraja hicho kwa sasa tayari kimevunjika na kusababisha usumbufu mkubwa wa usafiri na usafirishaji baina ya vijiji hivyo na Mji wa Chake Chake.

Je, ni lini serikali itawakomboa walipa kodi wa vijiji hivyo kwa kuwajengea daraja ya kisasa katika eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 25 kama hivi ifuatavyo:

Ni kweli kwamba wananchi wa Ng'ambwa, Gombani ya Kati Simwambili na Gawani wanategemea sana njia hii anayolalamikia Mhe. Mwakilishi ili waweze kuunganishwa na barabara kuu ya Chake Chake hadi Wete ikiwa kama *feader road*, ingawa hali yake kwa sasa inapitika ila tatizo kubwa ni kivuko hasa kwa vyombo vya moto kwa sababu *calvat* yake imechoka na imeshaharibika. Pamoja na kwamba hili si jukumu la moja kwa moja kwa Wizara yetu ila kutokana na kadhia yenyewe na kwa kuwa tayari tumefanya mazungumzo na wenzetu wa Halmashauri na wametueleza juu ya ugumu wa hali yao ya kifedha.

Aidha kwa nia ya kuwaondoshea wananchi hao usumbufu unaowakabili, Wizara yangu imepanga kujenga *calvat* mbili pacha yaani *twin pipe calvat* kwenye eneo alilolitaja Mhe. Mjumbe kwa kutumia mfuko wa barabara kwenye bajeti ya mwaka 2014/2015. Kwa sasa wananchi hao wanatumia njia mbadala ya Gombani Kongwe ambayo haina usumbufu wowote wa usafiri.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu hayo ninalo swali dogo sana la nyongeza. Mheshimiwa kwa kuwa unataka kujenga *calvat* mbili sijui ni *calvat* za aina gani, lakini Mheshimiwa vijiji vya Gawani, Gombani kati pale pamoja na Simwambili ni vijiji vya kihistoria pale Pemba kwa sababu mpaka sasa hivi ni vijiji vyenye hazina kubwa ya ile kahawa ya Arabica ambao inapendwa sana kunywewa na huuza wale katika soko la Chake Chake kupitia katika *calvat* iko *Arabica coffee* ambayo watu wengi wanaipenda pale Pemba huwa inatoka Simwambili, Gawani pamoja na Gombani ya Kati.

Kwa sababu gari zinazopita na kahawa hii ni kubwa na *calvat* ni ndogo sana ile je, unaonaje Mheshimiwa Wizara yako ikafanya maarifa ikajenga daraja ya kisasa kusudi basi yale magari yanayorudi kule Gombani ya Kati, Simwambili, Ng'ambwa kuweza kupita vizuri na biashara yao pale katika daraja lile.

(b) Mhe. Mwenyekiti, je, isingekuwa vyema kwa serikali ikafanya haraka suala hili la kujenga daraja pale kwa sababu msimu wa mvua unakaribia na pale watoto wanaokwenda shule wanapata shida siku za mvua maana inaweza ikasababisha ajali pale za watoto wetu ambao ni tatizo kubwa na mvua za masika zinakuja hizi, je, isingekuwa vyema kwa serikali ikakata pua kuunga wajihi ikajenga haraka haraka katika daraja pale ili mvua ikinyesha wakapata kupita watoto wetu wa shule.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, swali la kwanza Mhe. Mwakilishi alitaka kujua ni *calvat size* gani na aina gani ambayo itajengwa katika eneo ambalo analilalamikia. Mhe. Mwenyekiti *calvat* tunazokusudia kujenga ni *calvat* ya *twin pipe* kwa maana ya kwamba ni *calvat* ambayo itakuwa na matundu mawili makubwa kuweza kuruhusu maji kupita michirizi yote miwili. Kwa sababu gani ninajenga hivyo, kwa sababu eneo unalolalamikia ni barabara ya ndani tukisema tujenge daraja itatulazimu kwanza tuanze kutanua hilo eneo lenyewe la kupitisha maji jambo ambalo itakuwa si matumizi mazuri ya fedha.

Lakini suala la pili, umezungumza kwamba kwa kuwa tunakwenda katika kipindi cha mvua unaonaje serikali isiharakishe ujenzi katika daraja hilo. Mhe, Mwenyekiti kama maelezo yetu ya awali tuliyoyajibu kwamba kwa

kuwa tunatambua njia hii sasa hivi haipitiki kutokana na tatizo hilo la *calvat*, sisi kama Wizara tayari tokea mwaka jana tumeshafanya matengenezo makubwa kwa barabara ya ndani inayotoka Gawani, Gombani hadi Mkoroshoni, ambayo inaungana na barabara ya Kianga.

Na kwa kutambua kuwa wananchi wetu watapata usumbufu tumemshauri Mhe. Mwakilishi na wananchi tayari wanaitumia barabara ya Gombani ya kale kujinusuru kupita katika barabara hiyo ya Gombani ya sasa katika *calvat* ambayo ni mbovu. Kwa hivyo, imani yangu kwamba wananchi katika kipindi hicho cha mvua watatumia barabara hii ya Gombani ya kale ili kuweza kujinusuru na majanga yanayoweza kuepukika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibiwa swali langu kwa ruhusa yako, kwa kuwa leo ni tarehe 5/2/2014 ni siku ya kuzaliwa Chama cha Mapinduzi na kutimia miaka 37. Kwa hivyo, nichukuwe fursa hii kuwapongeza wanachama wa Chama cha Mapinduzi kwa kutimiza miaka 37 kwa chama chetu sambamba na kumpongeza Mhe. Issa Haji Ussi, kwa kutimia miaka 37. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti naomba swali namba 38 lipate majibu.

Nam. 38

Ujenzi wa Chelezo cha Kisasa Gati ya Pemba

Mhe. Saleh Nassor Juma Aliuliza:-

Katika kuimarisha usafiri wa baharini, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wawekezaji imeanzisha chelezo cha kisasa katika Bandari iliyopo Malindi kwa ajili ya *Ferry boats* sambamba na kujenga maeneo ya kukaa abiria wanaondoka na wanaoingia nchini bila usumbufu wa jua wala mvua, pamoja na kuwepo kwa eneo la wtu mashuhuri (*VIP Lounge*) la kisasa kabisa.Kwa kuwa huduma hii inapatikana Unguja na pekee na kwa kuwa Pemba nayo ni sehemu ya Zanzibar na huduma hii haiko wala haijulikani kabisa.

Je, ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaanzisha huduma hii katika kisiwa cha Pemba, aidha kupitia Serikali, ufadhili au kumruhusu Mwekezaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombino na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nizipokee pongezi, lakini bahati mbaya sijafikisha umri wa miaka 37. Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 38 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa kuona umuhimu wa kuimarisha huduma za abiria katika bandari za Pemba, ilijenga majengo ya abiria katika Bandari za Mkoani na Wete katika miaka ya 2006 na 2007, wakati huo huduma hizo hazikuwepo katika bandari kubwa ya Malindi Unguja. Ujenzi wa chelezo na majengo mapya ya abiria katika Bandari ya Malindi ulifanywa kwa udhamini mkubwa wa mfanyabiashara mzalendo.

Aidha kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha kutekeleza mradi kamahuo kwa Pemba, wizara yangu kupitia Shirika la Bandari inafanya mawasiliano na wawekezaji mbali mbali ili kupata ufadhili wa kuziendesha kwa kuziendeleza bandari za Pemba kwa ujumla ikiwemo kuanzisha huduma za chelezo.

Wizara yangu inamkaribisha muekezaji yoyote wa ndani au nje ya nchi mwenye nia na uwezo wa kuekeza katika kuziimarisha bandari za Pemba na Wizara yangu iko tayari kutoa kila aina ya ushirikiano katika kufanikisha jambo hilo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mbali ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba anieleze ni lini hasa bandari ya Mkoani itafanyiwa matengenezo kwa ajili ya hayo ambayo tuliyoyazungumza.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake. Kwa kuwa bandari ya Malindi ina sehemu mbili na ile sehemu moja iliyojengwa *terminal* ya abiria peke yake haipokei meli za mizigo imekuwa ni rahisi pale kuweka miundombinu ile kuilinganisha na bandari ya Mkoani sasa hivi. Bandari ya Mkoani inapokea kwa pamoja meli za mizigo na meli za abiria pamoja na boti.

Sasa kutokana na ukali huo uliopo au utata uliopo imekuwa ni vigumu kuweza kukupa tarehe hasa ambayo shughuli hiyo itafanywa kwa sababu unafanywa utafiti sasa hivi ni kwa njia gani zitawekwa taratibu hizo wakati mizigo vile vile iweze kushushwa na kuweza kupelekwa katika sehemu yake.

Kwa hivyo, tunakuomba Mhe. Mwakilishi, uwe na uvumilivu kama tunavyowaomba wananchi, mimi binafsi nimeshafanya mazungumzo na *Azam Marine* kwamba waweze kuitengeneza kama hapo. Na wao wameahidi wanafanya na wao *study* yao ili kuweza kuona pamoja na ugumu huo uliopo, lakini waweze kufanya utaratibu ili na abiria kule waweze kupata nafuu ya kupanda na kushuka boti.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, swali mama linaeleza kuwa katika kuimarisha usafiri wa baharini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wawekezaji imeanzisha chelezo cha kisasa katika bandari iliyopo Malindi. Mhe. Mwenyekiti, ndio kweli chelezo kile tulichonacho pale ni cha kisasa? Na kama ni cha kisasa ni sifa gani mpaka kiitwe chelezo cha kisasa.

(b) Kwa nini vyombo vyetu vinapotakiwa matengenezo makubwa wakati tunacho chelezo cha kisasa hulazimika kwenda katika chelezo cha Mombasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tunaposema chelezo kile cha kisasa maana yake ni uwezo wa chelezo chenyewe. Hadi muda huu chelezo kile hakijaweza kukamilika katika matumizi yake, chelezo kile kimejengwa kwa kukamilisha ile *Ramp* awamu ya kwanza ambapo wao wenyewe wametumia takriban shilingi milioni mia sita na ishirini. Awamu ya pili ya ukamilishaji chelezo kile ni kuchimbua eneo la kina cha maji, ili sasa utakapochimbua eneo la kina cha maji utawezesha sasa vyombo vikubwa kuweza kuja kufunga kwa wakati wowote.

Kwa sababu hivi sasa matumizi ya chelezo kile yanategemea *tide* ya maji, maji yanapojaa yanapokuwepo juu ndio unapata nafasi ya vyombo vikubwa kuweza kuviegesha katika chelezo. Na maji yanapokuwa yametoka hupata nafasi ya vyombo vikubwa kuviegesha katika chelezo kile. Kwa hivyo, katika hii awamu ya pili ya kuchimbua kina cha maji kikiongezeka tutaweza kutumia vyombo vikubwa kwa ajili ya kufungwa pale kwa wakati wote.

Swali la pili, kwamba kwa nini chelezo kile kipo vyombo visifanyiwe ukarabati katika eneo lile. Mimi nasema kwamba suala la kufanya ukarabati, chelezo kinachozungumzia kufanya ukarabati sio chelezo kile. Chelezo kile pale ni kwa ajili ya huduma ya vyombo vinavyokuja vya *Ro-Ro* pamoja na vyombo vyengine kwa ajili ya usafiri wa mizigo na abiria. Sehemu ya Karakana iko nyuma ambapo nako huko hivyo hivyo ikiwa kipindi cha maji makubwa vyombo vikubwa vinafanyiwa ukarabati. Kwa mfano kama meli ya *Sepideh* ni kubwa ambayo pia imefanyiwa ukarabati katika chelezo hicho hicho cha Karakana Kuu ya Bandari ya Malindi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anaongezea jibu la ziada pale alisema kwamba suala la kuweka *facilities* hizi katika bandari ya Mkoani inakuwa tatizo kwa sababu Unguja kuna sehemu ya bandari mbili ile ya abiria na ile ya sehemu ya mizigo. Sasa imeshindikana kuweka Mkoani kwa sababu sehemu ni moja tu, kama nimemfahamu kakusudia hivyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa aliyejenga *facilities* zile pale Malindi ni mfanyabiashara maarufu nchini ndugu yetu Said Salim Bakhresa, ameweka *facilities* nzuri pale na kwa taarifa tulizonazo anataka kufanya kitu kama kile katika kisiwa cha Pemba na tayari kwa mujibu wa taarifa tuliuzonazo ameomba apatiwe katika eneo la Wesha au Wete. Je, Mheshimiwa ni sababu gani za msingi ambazo zimepelekea serikali hadi leo hii kuwa na kigugumizi cha kuweza kumruhusu mfanyabiashara Said Salim Bakhresa kuweka kitu kizuri kama kile pale Wesha au Wete Pemba ni sababu gani za msingi.

(b) Mheshimiwa abiria wanaoingia na wanaondoka pale Pemba kupitia bandari ya Mkoani vile vile na wao wanaumizwa na mvua pamoja na jua linawaumiza sana na wao kwa sababu ni binaadamu. Je, ni sababu gani ya msingi kuendelea kuwaachia tu wale wakapata tatizo wakati wanapoteremka kwenda Pemba au wanapopanda meli kuja Unguja na sehemu nyengine kuendelea kupigwa na jua pamoja na mvua si kuwanyanyasa hawa raia wenu wa nchi hii jamani wakati mfanyabiashara eshaamua ajenge kitu kama kile ili na wao wasinyeshewe na mvua, kama hawa wa Unguja wasinyeshewe na mvua au wale wa kule Dar-es-Salaam, vile vile, na wao hawapigwi na mvua, je, mna hasadi hiyo serikali dhidi abiria kutoka Pemba.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti kwanza mimi katika maelezo yangu ya mwanzo sikusema kama imeshindikana nimesema *study* inafanywa kuona ni taratibu gani zitatumika kwa sababu gati ile ni ndogo tofauti na ya Malindi ambayo imeweza kubaguliwa ya kushusha mizigo mbali na hii *terminal* ya abiria boti ndogo na vyombo vidogo vidogo mbali. Kule gati iko mfumo mwengine ni nyembamba na haitaweza kubaguliwa kwenda ya mizigo na ya abiria. Kwa hivyo, *study* bado inafanywa ili kuona taratibu zote hizo zikikamilika, yoyote yule atakaekuwa amejitokeza atapatiwa fursa ya kuendeleza eneo hilo.

Swali la pili, yeye labda alisikia sikia tu kwamba bwana Bakhresa anataka kufanya hivi na hivi na hivi. Mimi nimezungumza *official* kabisa na uongozi wake yaani Meneja wake ambaye yuko Dar-es-Saaam na tukaelezana nia hiyo wanayo, lakini hawajakuwa tayari, siku watakaokuwa tayari na *study* yao ikakamilika, Wizara itatoa ruhusa moja kwa moja ya kujenga. Mimi sikusikia maneno nasikia sikia, mimi nimezungumza nao *official* moja kwa moja. Ahsante.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa ajili ya kuweka *hansard* sawa hiki ni chombo kikubwa sana lazima *hansard* zikae sawa. Wakati Mhe. Waziri kazungumza Hussein, mimi nimezungumza na mwenyewe Mzee Said

Salim Bakhresa hapa Unguja na akanambia yeye mwenyewe kapeleka maombi mawili hilo la Pemba kwamba aruhusiwe kujenga hii chelezo Wesha pamoja na Wete, lakini hajapata majibu, sambamba na kupatiwa sehemu ya kujenga Ofisi pale Malindi ambapo Ofisi yake ni ndogo pamoja na kuisaidia serikali, mpaka sasa wameshindwa kumpatia angalau sehemu, haya maombi mawili alinieleza mwenyewe Mzee Said Salim Bakhressa. Sasa tuwekeni *hansard* sawa tu.

Nam. 39

Tatizo la Ugonjwa wa Ndui kwa Wafugaji Mkoa wa Kaskazini "A"

Mhe. Panya Ali Abdalla: (Kny. Mhe. Kazija Khamis Kona) – Aliuliza :- Wafugaji wa kuku hasa katika maeneo mbali mbali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja wamekuwa wakijitahidi katika shughuli zao za ufugaji na wanazalisha vifaranga kwa wingi, hata hivyo vifaranga vingi hupoteza maisha baadae kutokana na tatizo la ugonjwa wa Ndui.

(a) Ni nini hasa chanzo cha ugonjwa huo wa Ndui.
(b) Wizara imejipanga vipi kukabiliana na tatizo hili ili kuwapa faraja wafugaji wetu.

Mhe.Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-.

Mhe. Spika, kwa idhini yako nakuomba uniruhusu kwa dhati kabisa kuwapongeza wanachama wa Chama cha Mapinduzi kwa kufika miaka 37 ya kuzaliwa Chama hicho. Lakini pili, nimpogeze ndugu yangu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kwa kuteuliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa tiketi ya CCM Jimbo la Kiembesamaki.

Mhe. Mwenyekiti na naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 39 lenye kifungu a na b kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ugonjwa wa Ndui ni maradhi yanayowaathiri kuku na bata mzinga na husababishwa na virusi (*Antipoxvirus).* Ugonjwa husababisha sehemu zisizo na manyoya kama vile kichwani zikijumuishwa upanga na ndewe kufanya vidonda vidogo vidogo ambavyo huishia kufanya vigaga vikavu na hatimae vidonda hivyo hupona haraka iwapo vitawahiwa kutibiwa. Wakati mwengine vidonda vinaweza kuenea katika njia ya chakula na njia ya pumzi na hii hutokea mara chache na hasa katika wale vifaranga wadogo sana. Ugonjwa huu umeenea dunia nzima na haujitokezi mara kwa mara

iwapo mfugaji atachukua hatua madhubuti ya ufugaji bora ikiwemo kufuata utaratibu wa kuchanja kuku kila ifikapo muda wake.

b) Wizara yangu inaendelea na kuwaelimisha wafugaji wa kuku na bata mzinga kuhusu umuhimu wa kuipatia chanjo mifugo yao na sio kusubiri hadi pale maradhi yanapojitokeza ili kuepuka hasara ambazo si za lazima. Nawashauri wafugaji wawe karibu sana na watoa huduma za mifugo na kuwaeleza maradhi yanapojitokeza ili wazidi kupata ushauri mzuri juu ya namna bora ya kuikinga mifugo yao na maradhi mbali mbali yanayojitokeza. Aidha dawa za chanjo zipo na zinapatikana hapa Zanzibar bila matatizo yoyote.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali la nyongeza lenye (a) na (b). Kwa kuwa ugonjwa huu wa ndui ameshauelezea, lakini pia kuna ugonjwa wa mahepe ambao unawasumbua sana wafugaji kwa kupoteza kuku wao wengi, je, Mhe. Waziri ni vipi unawapa elimu wafugaji wetu hawa kuhusiana na ugonjwa wa mahepe.

Lakini (b) kuna wafugaji wa kuku wengi ambao wanafuga na kuku wao kwa kweli wanatotoa sana mayai, lakini wanachangamoto la kutoangua mayai hayo. Je, serikali inawasaidia vipi wafugaji hawa ili kuwapatia mashine ya kutotoleshea vifaranga ili waweze kuzalisha vifaranga kwa wingi ikiwa ni hatua moja ya kuweza kujiondosha katika umaskini.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli ugonjwa wa mahepe upo, lakini bado wizara yangu inatoa ushauri ule ule kwa wafugaji wetu wachukue hadhari za kutosha ili basi kuchanja kila muda unapofikia na vile vile hakuna *cross infection* kati ya ugonjwa wa ndui na ugonjwa wa mahepe. Hivyo, basi tutaendelea kutoa ushauri na wataalamu wangu watafika mara kwa mara vijijini ili kutoa ushauri huo. Lakini swali la pili ni zuri tutalichukua na tutalifanyia kazi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Mwenyekiti, katika kutoa majibu Mhe. Waziri, alisema kuwa maradhi haya ya ndui yanaingia kwenye kuku kwa zile sehemu ambazo hazina manyoya. Tunayo kabila ya kuku, lakini kisayansi siijui wanakuwa hawana manyoya isipokuwa kidogo tu, lakini wanapoingiwa na ndui huwa ni kwenye uso tu na zile sehemu zilizo wazi huwa hazipati maradhi hayo kwa nini.

Pili, kwa sababu tunaambiwa kinga ni bora kuliko tiba kwa nini Wizara haioni umuhimu wa kutafuta chanjo za kinga ya maradhi haya ya ndui kwa vifaranga vyetu ili wakulima au wafugaji wasiathirike.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme tu katika jibu langu mama nimesema ugonjwa huu unaathiri sana sehemu za kichwa, ndewe na sehemu za upanga zisizo na manyoya. Wale kuku ambao amesema yeye wanaitwa vipotugali, lakini kila ugonjwa una sehemu zake na una athari zake. Nizungumzie kama *TB*, *TB* sana inaweza ikaanza kwenye kifua, iko *TB* ya mifupa na sehemu nyengine. Lakini huo ugonjwa wa ndui hizo ndio sehemu zake *specific* ambazo zinaweza zikaathiri kuku.

Lakini hili la pili, nimezungumza katika jibu langu kwamba msingi kuwa dawa za chanjo zipo Zanzibar zinapatikana bila ya matatizo yoyote. Tuwashauri tu wafugaji wetu waweze kutumia chanjo hizi ili kuweza kupata mifugo bora isiyoweza kuathirika mara kwa mara.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana, Mhe. Mwenyekiti na mimi kuniona kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, wafugaji wengi wa kuku, kuku wao wanapopata magonjwa ama ni ndui au mahepe au ugonjwa mwengine wowote dawa kubwa wanayoifanya ni kuwachinja na kuwala. Je, kwa kuwa kuku wenyewe ule ugonjwa hatimaye wanasabisha kifo, hakuna madhara yoyote kwa mfugaji kumla kuku yule.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, hakuna tafiti yoyote iliyofanywa kwa sasa na kuona kuwa maradhi yale yanaweza yakasababisha vifo kwa binaadam.

Nam. 40

Kutokamilika kwa Ujenzi wa Soko la Kidaazini

Mhe. Panya Ali Abdalla (Kny: ya Mhe. Kazija Khamis Kona) – Aliuliza:-

Katika kuhakikisha kwamba wavuvi wa maeneo ya Kidaazini huko Wilaya ya Kaskazini ‘A’ wanafanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi. Serikali kupitia Idara ya Uvuvi na Mfuko wa *TASAF* imeamua kujenga soko la kisasa katika eneo hilo, lakini hivi sasa halijakamilika.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea kutokamilika kwa ujenzi huo.
(b) Ni lini ujenzi wa soko hilo utakamilika ili wavuvi wa sehemu hiyo walitumie ipasavyo soko hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: - Alijibu:- Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Kazija Khamis Kona swali lake Nam. 40 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjuilisha tu Mhe. Mwakilishi kwamba Soko la Kidanzini lilijengwa kwa ufadhili wa *MACEMP/ TASAF*, pamoja na masoko mengine ya Mazizini na Kizimkazi Dimbani. Wakati ilipoanza kazi ya ujenzi huo kwa wavuvi wa Kidaazini walipendekeza mabadiliko ya ujenzi uliokusudiwa, na fedha zilizokusudiwa pale zilikuwa ni shilingi milioni 30, lakini yale mapendekezo ambayo walipendekeza kilizidi kiwango kile walichoomba. Sasa *MACEMP/TASAF* tayari ilishatoa pesa zile milioni 30 ili kutekeleza ujenzi ule. Naomba niushauri tu uongozi wa Soko la Kidanzini kutafuta ushirikiano na wadau mbali mbali ikiwemo pamoja na serikali kwa kumaliza ujenzi husika.

(b) Sehemu iliyosalia itakamilishwa na kutumia vifungu vya wizara pale ambapo hali ya fedha itakaporuhusu, pamoja na michango ya wao wenyewe wavuvi, halmashauri na viongozi wa jimbo watumie Mfuko wao ili kuondoa kadhia kubwa ile ya wananchi wao wa pale.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

(a)Kama ilivyodhihirika jana wakati tunajadili Ripoti ya *PAC*,inaonekana miradi mingi hii ya ujenzi wa masoko na mambo mengine yanayosimamiwa na *MACEMP* imekuwa na matatizo kutokamilishwa au kujengwa chini ya kiwango. Ni sababu zipi zilizopelekea *MACEMP* ikawa na maradhi haya ya kudumu.

(b)Wizara yake inachukua hatua gani kwa uongozi unaosimamia miradi hii ya *MACEMP* ambayo imeacha kadhia kama hizi katika kila maeneo kwenye Visiwa vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naomba arudie swali la (a) sikulifahamu vizuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, swali langu (a) nilikuwa nasema kama tulivyoona jana wakati tunajadili Ripoti ya *PAC* miradi mingi ambayo iko chini ya *MACEMP* katika Idara hii ya Uvuvi inayohusu ujenzi wa masoko na vituo vya wavuvi inaonekana ina matatizo, kama ilivyoonekana jana katika eneo la Chumbe, lakini pia ofisi ya idara kwa upande wa Pemba

na leo tunaliona hili jengine. Nikasema ni zipi sababu zinazopelekea miradi inayohusiana na *MACEMP* kusibiwa na maradhi kama haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme nikubaliane naye moja kwa moja kuwa miradi mingi ilipoachwa kwa wananchi imekuwa haifanyi vizuri. Hivyo basi, wizara yangu kama kwenye soko la Tumbe na masoko mengine imechukua tahadhari kwa kutumia vile vifungu vyake na kuweza kumaliza, lakini hali inaporuhusu kifedha.

Hili jengine tumeiona kadhia hii sana, na nasema wizara imechukua hatua madhubuti kwa kuweza kurekebisha hatua zile zinazoweza kurekebishwa. Lakini hata hivyo, ni miradi mingi iliyoachwa kwa wananchi imebaki kudorora wenyewe, hivyo basi, tuweze kutoa elimu ya kutosha na kuweza kuhifadhi hii miradi ambayo yenye pesa nyingi za nje na ambazo zimeweza kutumika.

(b) Miradi mingi sasa hivi iliyobaki tumeanza kuichukua, tumeanza kutafuta mmoja baada ya mmoja. Tumesema kuuchukua ule wa Tumbe ambao soko kubwa la Tumbe tumechukua fedha zile ambazo tulikuwa tumempa mfadhili ili tuweze kujengea pale yule *contractor* ambaye amebakia, lakini hii mingine ambayo ipo tutafanya utaratibu wa kuitizama ipi iliyobaki na tuweze kuichukua kuifanyia kazi hatimaye kuweza kuimaliza yote, lakini kwa sasa hatujaweza kuimaliza.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, swali langu (b) lilikuwa ni kwamba, uongozi wa wizara yake unachukua hatua gani kwa wanaosimamia hii miradi ya *MACEMP* ambao wamesababisha matatizo haya, sio kwamba itafanya hatua gani kukamilisha hii miradi. Wale wanaosimamia miradi hii ya *MACEMP* ambao wamesababisha matatizo kila pahala mambo kama haya ya kujenga chini ya viwango na kutokamilisha ujenzi. Uongozi wa wizara unachukua hatua gani kwa watu wale? Ndio swali langu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, labda kwa kuongezea tu kama alivyouliza Mhe. Mjumbe pale kuwa wizara imechukua hatua gani. Wizara hatua ya mwanzo ambayo ilichukua ilimzuia yule *contractor* na imezuia zile shilingi 50 milioni zilizobakia hatukumlipa, matokeo yake tumekaa na wahusika wa Tumbe pamoja na mwenyewe ili kuona kwamba tunashirikiana pamoja; baina ya *contractor* na wadau wa pale Tumbe wenyewe. Pesa hatukummalizia baada ya kuona kwamba kazi aliyoifanya haikuturidhisha. Hii ndio hatua moja muhimu ambayo tumeichukua.

Baadae tutaangalia je, kuna hatua ya kumpeleka mahakamani au vipi? Lakini hatua ya kwanza tumezuia zile shilingi 50 milioni hatukumlipa. Bado hatujazipata zile pesa lakini itabidi lazima tuzidai. Kwa sababu mpaka sasa hatujazipata kutoka *World Bank, ECO Bank***,** lakini tumemuomba Mwanasheria Mkuu atupe utaratibu wa kisheria tuone namna gani tunazipata zile pesa ili tukae na wadau wa Tumbe tuone kwamba tunamaliza zile kasoro zetu zilizobakia pale. Lakini kwa upande wa *contractor* tumemzuia pesa hatukummalizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri pamoja na Waziri kwanza kabisa na mimi nilikuwa nataka nijipongeze, lakini na mimi vile vile mnipongeze. Kwa sababu nilizaliwa Chaani Steni tarehe 05/02/1965. Sasa leo ni siku yangu ya kuzaliwa. Kwa hiyo, nashukuru kwa wale ambao wameamua kunipongeza naamini na zawadi nyengine zitakuja baadae.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa miradi mingi ya wananchi kama ilivyoelezwa hapa kupitia miradi ya *MACEMP,* lakini vile vile na miradi mingine ya *TASAF* huwa inashughulikiwa lakini inakwama katikati kutokana na ufinyu wa bajeti. Na kwa kuwa masharti ya hawa wahisani miradi kama hii inakuwa inatengewa fungu, kwa mfano kwa miradi hii tuseme kama shilingi 30 milioni.

Je. wizara walipofanya uchambuzi yakinifu na akaona zile fedha hazitotosha hawaoni iko haja kuanza kuwahamasisha wananchi. Lakini vile vile kupitia Mifuko mingine ili kuhakikisha ule mradi unapoanza mpaka unamaliza kuliko hivi ilivyo hivi sasa kuwa miradi huwa inafanywa lakini inaishia katikati. Mhe. Waziri haoni hivi sasa kama mtaanza miradi kwanza kuangalia bajeti, mchanganuo na halafu baadae ule mradi ukianza mpaka umalizike.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mhe. Hamza Hassan Juma kwa siku yake ya kuzaliwa baadae tuungane pamoja katika kusherehekea siku hiyo.

Vile vile katika suali lake ni kweli imeonesha wazi sana katika miradi mingi waliyopelekewa wananchi imeweza kuwa haifanyi vizuri. Sasa wizara yangu inafanya *feasibility study* kwanza na tuangalie bajeti yetu na kile ambacho kinahusika, ili tuweze kuwapelekea wananchi pamoja na kuwapa elimu ya kutosha kuweza kutumia Mfuko ule tuliokuwa nao kwa urahisi na kujua basi kitu gani kitamalizika kwa wakati.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika kutoa majibu Mhe. Waziri alisema kuwa lile soko mwanzo ambalo lilifadhiliwa na *MACEMP* na *TASAF* lilikuwa lijengwe kwa pesa za Kitanzania shilingi 30 milioni, lakini badala yake kukatokea ubadilikaji wa plani na fedha ikaongezeka.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea ikawa plani ya mwanzo ikafeli ikaja plani nyengine. Vile vile baada ya plani hiyo mpya ni kiasi gani cha fedha zilizoongezeka ili mradi huo ukamilike.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa wananchi wenyewe ndio walileta mabadiliko yale kutokana na soko lile kuwa dogo ili waweze kupanuliwa kuwa kubwa zaidi ndio *amount* hii ikaongezeka. Lakini vile vile kuwa ni kiasi gani kwa sasa siwezi kukupa takwimu nitaweza kukujibu kwa maandishi.

Nam. 4

Upandaji wa Maji ya Chumvi Katika Maeneo ya Wananchi

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:

Mhe. Mwenyekiti kabla ya kujibiwa swali langu naomba nifanye marekebisho kidogo, pale palipoandikwa Bonde la Maotwe iongezeke Kangani. Ahsante.

Hivi sasa katika Wilaya ya Mkoani kumejitokeza hali ya maji ya bahari, kupanda maeneo ya juu na hasa kwenye mashamba ya wananchi, ikiwemo Bonde la Maotwe ambapo mashamba yafikayo 100 yamevamiwa na maji hayo, na hivi sasa tayari msimu wa kilimo cha mpunga umewadia. Kutokana na hali hiyo kuna wananchi wamejitokeza kulima matuta ili kuzuia maji hayo.

(a) Je, serikali imejipanga vipi kuyazuia maji hayo yasisambae na kusababisha athari kwa wananchi wa maeneo hayo.

(b) Je, ni zipi athari za maji chumvi kupanda katika mashamba ya wananchi.

(c) Je, serikali inachukua hatua gani kuwasaidia wananchi hao wanaoathirika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima kwa kuweza kufika katika Baraza hili tukufu na kutekeleza shughuli zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeweza kuyaorodhesha maeneo yote yanayoingia maji ya chumvi kwa lengo la kuchukua hatua zinazofaa ili kupunguza kasi ya athari ya tatizo hili. Aidha, serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaendelea kuhamasisha na kushirikiana na wananchi katika kuwaongoza ili waweze kujenga matuta na kuzuia tatizo hili la maji ya chumvi kuvamia eneo la kilimo na makaazi.

(b) Athari za maji chumvi kupanda katika mashamba ya wananchi ni kama ifuatayo: Kupungua kwa maeneo ya kilimo na makaazi ya watu, kupungua kwa mavuno katika mashamba yanayolimwa, kuanguka kwa uchumi ambapo hupelekea jamii kukosa lishe bora na kuongezeka kwa umasikini, kupotea kwa Bio anuai ya nchi pamoja na viumbe wengine.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa gharama ya kujenga matuta katika maeneo yote yanayoingia maji chumvi ni kubwa. Hata hivyo, serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili imejenga matuta ya kuzuia maji ya bahari kuingia katika mashamba ya wakulima mita 250 bonde la Machamawe, mita 400 bonge la Koowe, Ukele mita 900, Tumbe Magharibi, Vualeni mita 400, Kengeja kwa Jibwa mita 200. Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo pamoja na taasisi nyengine, bado inaendelea kutafuta wafadhili ili kuweza kusaidia kukabiliana na athari zinazotokana na uvamizi wa maji ya bahari katika maeneo hayo. Ni imani yetu kwamba, katika maeneo ambayo tayari tumeshajenga matuta wananchi watayatunza na kuyaendeleza ili yadumu kwa muda mrefu na kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsane sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Mara nyingi wananchi hutegemea serikali yao kuweka hakiba ya chakula cha kutosha ili yatokeapo majanga kama haya serikali iweze kuwasaidia.

Je, serikali imejipanga vipi kwa hili, pale ambapo mashamba yatakosa kuotesha mazao kutokana na kuathirika kwa maji chumvi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kupitia katika mpango wa chakula na lishe suala hili tayari tunalifanyia kazi ili kuwa na mpango wa kuweka hakiba. Hivi sasa kama tulivyokuwa tuna mchakato mzima wa kukarabati maghala ambayo tunataka kuwekea chakula, na mtiririko mzima tayari tumeshaufanya kupitia kufanya tathmini katika kila shehia. Kwa hivyo, kilichobakia sasa kukarabati maghala ambayo hivi sasa tushakabidhiwa ili kuweka mpango wa chakula cha hakiba katika nchi yetu.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri, na kama alivyosema katika jibu lake la msingi kuwa fedha zinazotolewa katika kujenga matuta haya ni nyingi, na wizara yake ndio iliyokuwa ina wataalamu wa kuwatoa katika kusimamia ujenzi wa matuta haya, na tulifika pahali kuona kuwa kuna bonde lile alilolitaja moja la Ukele kujengwa katika kiwango kisichokuwa cha ubora.

Je, Mhe. Naibu Waziri wizara yake ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa fedha hizi zinapotolewa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wanatoa wataalamu waliokuwa wana uhakika na ujuzi wa kujenga masuala ya matuta haya katika kuzuia maji ya chumvi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, suala la kujenga matuta ya ubora kama tunavyojua wizara yangu ina wataalamu wa kushughulikia masuala haya. Kwa hivyo, suala la tuta alilolisema tutajitahidi kutafuta wataalamu wazuri ili matuta haya yakae vizuri kwa kuzuia tatizo hili lisije likarejea tena.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri ametueleza kuna maeneo mengi ambayo yanaingia maji chumvi na yameorodheshwa katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Sasa naomba Mhe. Naibu Waziri anifahamishe ni maeneo mangapi kwa Unguja na ni mangapi kwa Pemba ambayo yamevamiwa na maji chumvi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, maeneo ambayo yaliorodheshwa Unguja na Pemba, maeneo ya Pemba 123 na maeneo ya Unguja 25, yote 148.

Nam. 45

Bajeti Kutozingatia Wakulima wa Maweni

Mhe. Asha Abdu Haji – Aliuliza:

Imekuwa ni kawaida kwa Wizara ya Kilimo na Serikali kwa ujumla wakati zinapozungumzia au kutayarisha matumizi au Bajeti ya Kilimo (katika mashamba) huwa zinazingatia zaidi kilimo katika mabonde ya mpunga na maeneo mengine yasiyokuwa ya maweni.

(a) Kwa kuwa visiwa vyetu kwa upande wa kilimo vimegawika katika sehemu za maweni na sehemu zisizokuwa za maweni. Je, kujadili au kujihusisha na kilimo kwa sehemu zisizokuwa za maweni tu na kuzisahau (kuziacha) sehemu za maweni itakuwa ni kuwatendea haki wakulima wa maweni.

(b) Ikiwa jambo hilo si kuwatendea haki wakulima wa maweni. Je, Wizara ya Kilimo na Serikali kwa ujumla zinazungumzia nini juu ya kuwasaidia wakulima wa maweni.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 'a' na 'b' kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo na Maliasili inawatendea haki wakulima wa maweni kama wanavyotendewa haki wale wasio wa maweni, kwa kuwapatia fursa zote zinazotakiwa ikiwemo kuwapeleka ziara za kimafunzo, kushiriki katika maonesho ya shamba darasa pamoja na kuwapatia huduma muhimu za elimu kwa wakulima.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo kupitia Kitengo chake cha Mbegu pia huzalisha mbegu ya Mahindi, Mtama na Kunde na huzisambaza vituoni kwa ajili ya wakulima wa maweni, ingawa mbegu hizi kwa kiasi kikubwa huwa hazinunuliwi zinapopelekwa vituoni na kupelekea kuharibika ghalani.

Aidha, wizara itaendelea na juhudi za kuwaelimisha na kuwasaidia wakulima wa maweni kwa hali na mali kwa ajili ya kuleta maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri namuuliza Mhe. Naibu Waziri je, ni wakulima wangapi ambao washapata mafunzo katika Wilaya ya Kusini, wanawake ni wangapi na wanaume ni wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ni suala ambalo linatakiwa idadi kamili na sikuweza kuorodhesha wale wakulima wote waliopatiwa mafunzo kwa kuwa ni wengi, basi naomba nimjibu kwa maandishi swali lake hili.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Wazanzibari wote takriban asilimia kubwa wamewekeza katika kilimo ikiwa ndio mfumo wa maisha yao, na kwa sababu Zanzibar imeingia katika uwekezaji, na ardhi kubwa hivi sasa ni maweni na isiyokuwa ya maweni imepewa wawekezaji kwa kuwekeza mambo ya mahoteli na mengineyo na ardhi hiyo inapungua kwa wingi na idadi ya watu inaongezeka.

Je, Mhe. Naibu Waziri ana ushauri gani kwa serikali wakati wananchi wanategemea kilimo, ardhi inaingizwa katika mambo ya utalii, ardhi inapungua na watu wanaongezeka na watu wetu hawa masikini itakuwa hawana mfumo wa maisha, ana ushauri gani kwa serikali kuhusu mambo haya.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, ardhi imepangwa katika mpango maalumu wa matumizi ya ardhi; kuna maeneo ya kilimo, kuna maeneo ya utalii, kuna maeneo ya ujenzi. Tunachotakiwa kufanya ni kuwaelimisha watu wetu kwamba wasiwe wanakimbilia pesa, wajue kwamba wanapopauza hapahusiki na masuala ya utalii basi pasiuzwe kwa ajili ya utalii patumike kwa ajili ya kilimo. Wizara yangu inajitahidi katika kuwaelimisha wananchi juu ya suala hili.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mbegu ya mpunga wakulima wanauziwa kwa bei ya ruzuku. Je, wakulima wa maweni mbegu ya mtama, kunde na mahindi wanauziwa kwa bei gani na bei hiyo ni ya ruzuku.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, mbegu ya mtama wanauziwa wakulima kwa bei ya shilingi 1,000 kwa kilo. Mbegu hii hawauziwi kwa bei ya ruzuku, ila mpunga tu ndio tuliouweka bei ya kuuziwa wananchi kwa ruzuku. Kwa sababu ni kilimo kinacholimwa na wananchi wengi.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla sijamkaribisha na kumtaka Mhe. Saleh Nassor Juma aulize swali lake muda wetu wa maswali unakaribia ukingoni. Na kwa asubuhi hii ya leo shughuli yetu ilikuwa tunamaliza maswali tu baadae tutaondoka ili kurejea jioni kwa ajili ya kupata hitimisho. Tungelimuomba basi na nikuombeni Wajumbe tuongeze muda kidogo kwa mujibu wa Kanuni ya 39(3) ili tumalize haya masuala yetu mawili matatu tuliyonayo, baadae tuweze kuakhirisha Baraza na jioni tuje kukamilisha ufungaji wa Baraza letu hili. Nimuombe basi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili tuweke kanuni kando tuweze kumalizia haya masuala baadae tuendelee na utaratibu wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa robo saa iko ndani ya uwezo wako tunaweza kuendelea na Baraza kwa robo saa.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Nam. 32

Kufanyiwa Vipimo vya Afya kwa Wageni kwenye Miradi ya Ujenzi

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Miradi mikubwa kama vile ya ujenzi wa Miundombinu mbali mbali ikiwemo ya barabara ambayo mara nyingi hutoa zabuni kwa Kampuni za Kigeni, kwa kuwa wafanyakazi wa Makampuni hayo mara wanapotumia muda huo kwa shughuli mbali mbali katika miji na vijiji vyetu ikiwa ni pamoja na mashirikiano ya hali ya juu na jamii iliyowazunguka bila kujali jinsia, tendo ambalo mara nyingi hupelekea suala zima la kujamiiana.

je, ni lini serikali itachukua hatua ya kufanya vipimo kwa wageni wa nchi hii kama vile tunavyofanyiwa Watanzania tunapoingia katika baadhi ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Alijibu :- Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake Nam. 32 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kauli mbiu ya ulimwengu hivi sasa kuhusu UKIMWI ni *zero* tatu. *Zero* ya kwanza inahusu maambukizi mapya yasiendelee, *zero* ya pili inahusu vifo vitokanavyo na UKIMWI je havipo? na *zero* ya tatu ni kuhusu unyanyapaa wa wanaougua UKIMWI uwe haupo. Ili maamuzi haya yachukuliwe na serikali, kunahitajika sera na miongozo baada ya kuzingatia kwa kina faida na hasara yake. Hata hivyo, nchi chache kwa sasa ambazo

hulazimisha mtu kupimwa VVU kabla ya kuingia na nchi nyingi duniani ikiwemo Marekani zimekuwa zikijaribu kuondoa sheria hii, kwani inaonekana kuleta malalamiko yanayohusishwa na unyanyapaa.

Kwa vile Tanzania ni waumini wa *zero* tatu, kutunga sera kama hiyo si sahihi kwa sababu serikali yetu inapinga unyanyapaa kwa watu wanaoambukizwa Virusi vya UKIMWI au Ugonjwa wa UKIMWI.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika swali langu la msingi nimeuliza kwamba hawa *contractors* au makampuni mbali mbali wanapokuja kufanya kazi hapa watendaji wake wanakuwa na maingiliano makubwa sana na raia wetu bila ya kujali jinsia, jambo ambalo maingiliano haya yanaweza yakapunguza sana kufikia *zero* tatu. Kwa sababu yanaweza yakapelekea mpaka matendo ya kujamiiana. Kwa kuwa sisi tunapokwenda nje ya nchi Wazanzibari hulazimika kufanyiwa *medical checkup* kikiwemo mpaka kipimo cha UKIMWI, mimi nadhani na wao kuwapima haitakuwa unyanyapaa, bali tutapata muda mzuri wa kuja hapa na kuwapa ushauri nasaha tukishawajua kama wameathirika tutawapatia madaktari kuwapa ushauri nasaha.

(a) Je, tukiwaachilia waingie wakiranda katika maeneo mbali mbali wakiingia huku wakitoka kule na baadae kufanya matendo kama hayo , sasa hizo zero tatu tutazifikia.

(b) Tunapokwenda nje tupimwe na nchi nyengine unaambiwa kuwa kama huna kipimo basi urudi. Tuseme na sisi tunanyanyapaliwa na nchi hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: (a) Kwa *nature* hilo suala lake analoliuliza linategemea zaidi *contract* zinapofanywa kwa watu kuja kujenga au mambo mengine yoyote yanayofanywa. Katika moja ya masharti yake si kupima ukimwi. Kwa hiyo, watakaokuja wakiwa wamepata *contract* kwa sababu ndizo zinazotolewa na wakifuata taratibu zote za *contract* ukiwa haumo watapata tenda na watakuja hapa kufanya shughuli zao wanazozifanya.

Suala la maingiliano ya kimwili na mengineyo hayo yanategemea wenye *contract* wanaokuja na wale walioko pale, halina ulazima hilo. Sasa kama waliopo wenyeji wameona kuwakaribisha wageni wao ndio kufanya hayo sasa hilo ni jukumu lao wao wenyewe. Kwa sababu hakuna asiyefahamu kwamba yakifanyika hayo mtu anaweza akapata ukimwi. Kwa hivyo, mimi ningependa kuwaasa ndugu zangu ili tuepukane na ukimwi madhali watu

hatuwafahamu na hawakupima ukimwi basi tujiepushe kufanya hayo yanayofanyika ili kuepusha ukimwi.

Lakini hatuwezi kuwazuia ambao waliokuja na waliowakaribisha wakakubali kufanya hivyo halafu tuseme kwamba tuwapime ukimwi. Hilo haliwezekani kwa sababu sera ya nchi yetu hairuhusu hili.

(b) Tunapokwenda kwenye nchi mara nyingi wanaopima ukimwi ni wale wanaokwenda kwa muda mrefu. Aidha unakwenda kusoma kwa kipindi kirefu au unakwenda kuishi, kwa muda mfupi hatujapimwa ukimwi. Kwa hiyo, utachagua kama unataka kwenda upime ukimwi katika hiyo nchi. Kwa hiyo,unapoambiwa kupima ukimwi uchaguzi ni wako. Mimi nimeenda kusoma nimepimwa ukimwi, lakini nimeshakwenda nchi nyingi kwa muda kwa sababu hizo ni sera zao na maamuzi ni yako na wewe pia una maamuzi.

Nam.47

Usumbufu wa Kupatiwa PF3 Kwa Waathirika wa Ajali

Mhe. Asha Abdu Haji: Aliuliza:-

Katika maisha ya kawaida binaadamu wanaweza kupata ajali iwe zimewatokea wao wenyewe au zimesababishwa na watu au mambo mengine, mara nyingi zinakuwemo ajali ambazo zinasababishwa na uzembe, hivyo basi kwa aliyejeruhiwa hukataliwa kutibiwa mpaka apate karatasi No. 3 ya Polisi *PF3* kutoka katika kituo cha Polisi na mara nyengine upatikanaji wake huwa na usumbufu mkubwa jambo ambalo humuachia aliyejeruhiwa kuendelea kupata maumivu makubwa

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba unipe idhini tena na kumjibu Mhe. Asha Abdu Haji swali lake namba 47 kama hivi ifuatavyo.

Dhana ya kutotibiwa kwa mtu aliyepata ajali au majanga ya aina yoyote kwa kukosa fomu namba 3 ya Polisi PF3 anapofika hospitali. Kwa kawaida mgonjwa wa ajali anapofika hospitali anatakiwa awe na fomu hiyo kwa ajili ya kujaza, lakini ikitokezea mtu aliyepata ajali amefika hospitali bila ya fomu hupatiwa matibabu kwamba kwa mujibu wa hali, na masuala ya kupatikana kwa fomu ya Polisi hufuatia baadae.

Iwapo mgonjwa hali yake inaridhisha na hatiliwi mashaka ya uhalifu baada ya kupatiwa matibabu daktari anamruhusu kurudi nyumbani na kufuatilia

masuala ya *PF3*. Ikitokezea mgonjwa kutiliwa mashaka yoyote ya kiuhalifu hospitali inafanya mawasiliano na Kituo cha Polisi kilicho karibu yake kwa uchunguzi zaidi.

Na kama hali ya mgonjwa yuko mahatuti jamaa wa mgonjwa hulazimika kufuatilia fomu hiyo ya Polisi kwa ajili ya kujazwa na kutoa ushahidi unaofaa wakati mgonjwa huyo anaendelea kupatiwa matibabu.

Naomba ikimbukwe kwamba utaratibu wa *PF3* umewekwa na Wizara ya Mambo ya Ndani. Hivyo basi hospitali huwa zinatekeleza tu utaratibu huu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Kwanza naomba nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na fasaha.

Nilikuwa naomba kuiuliza serikali tu kwa sababu mara nyingi yanatokezea malalamiko haya kwa wananchi kwamba inapotokezea na hali zikawa mbaya wanashindwa kupata matibabu kwa sababu ya kushindwa kutimiza masharti haya ya kuwa na fomu ya *PF3*. Hivi serikali haioni kwamba imefika wakati kama inavyoanzisha vituo vingi katika maeneo ya hospitali ili kupunguza matatizo mbali mbali na hili la kuwa pengine ama vituo au maofisa wa polisi katika maeneo ya hospitali kushughulikia malalamiko kama haya na kupelekea wananchi wanaopata matatizo kama haya waweze kutibiwa na kupata fomu za *PF3* pale pale katika maeneo ya hospitali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe.Mwenyekiti, nimesema katika jibu langu kwamba suala la *PF3* limewekwa na Wizara ya Mambo ya Ndani. Sisi watu kama wa hospitali tunatimiza hilo kwa sababu ndio maelekezo tuliyopewa. Sababu za msingi kesi, uhalifu na mambo mengine kama haya.

Sasa mimi nafikiri kuwa tutasema kwamba polisi waje wakae kwenye vituo vyetu na mahospitali sisi kama Wizara ya Afya sidhani kama tuna mamlaka hayo, lakini nafikiri walioko kama wataliona lina umuhimu maana vituo vya Afya na Hospitali ni nyingi, kwa hiyo kila pahala wakaweke Polisi wakae pale tu kwa kusubiri ajali, sidhani kama ni matumizi mazuri ya wafanyakazi tulionao.

Vituo vya Polisi vimeenea kila pahala viko karibu nchi nzima na sijawahi kusikia kwa upande wangu mimi wale waliokuja mara nyingi wakielekezwa kwenda wanachukua *PF3* wakati wakiwa wagonjwa wao wanatibiwa.

Pindipo ikiwa mgonjwa daktari kakataa kumtibu eti kwa sababu ya *PF3* hilo ni kosa na hasa kama hali yake ni mbaya, lakini pia kama mgonjwa ameshafika na tunamuona kuwa ni muhalifu huyu huwa tunapiga simu na

Polisi wanakuja pale, mara nyingi tu mimi nawaona kwenye mawodi wanawaangalia hao wagonjwa na wanachukua kitu wanachokitaka na wanajaza *PF3*.

Kwa hivyo, mimi nafikiri wanaohusika na hilo kama wataona litawasaidia basi bora wafanye hivyo, lakini sisi kama Wizara ya Afya hatuna uamuzi huyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, **Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nataka nikubaliane na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba upo umuhimu wa kuweka utaratibu ulio mzuri zaidi utakaowasaidia wagonjwa wetu hususan wale mahututi pale panapotokea tatizo ili matibabu yawezekane.

Huo utakuwa ni ushauri mzuri ndani ya serikali tukatizama zaidi hili kuwa na mpango pale pale Wizara ya Afya linapotokezea tatizo kwa wale waliopata ajali ghafla au mambo mengine ili ile huduma kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri iendelee na zile fomu ziwe zinajazwa pale halafu baadae zipelekwe polisi kwa ajili ya kupata taratibu nyingine. Maana vyenginevyo tunaweza kupoteza maisha ya watu wetu.

Kwa hivyo, nafikiri ni ushauri mzuri tutauchukua na kuufanyia kazi ili tuone utaratibu gani mzuri zaidi utakaotoa huduma hii kwa vizuri ili isitokezee matatizo kwa wananchi wetu pale wanapotokewa na jambo la dharura hasa inapotokea mambo haya ya ajali za ghafla na ikasababisha kwa njia moja au nyengine matibabu yasifanyike kwa wakati.

Nawashukuru sana Wizara ya Afya wanachukua hatua ya kutoa huduma hiyo pale mgonjwa anapokuwa katika hali hiyo lakini tutaliweka vizuri zaidi. Nakubaliana naye Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Nam. 36

Serikali Kuwajengea uwezo Makocha wa Mpira wa Miguu Wazalendo

Mhe. Nassor Salim Ali: Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa wakati huu inaonekana kwamba haina uwezo wa kuajiri Kocha wa Kimataifa wa mpira wa miguu hapa nchini, na kwa kuwa soka hapa Zanzibar bado linabakia kuwa chaguo la wananchi wengi hapa nchini bila ya kujali jinsia. Na kwa kuwa hapo zamani timu za Zanzibar ikiwemo Small Simba kupitia makocha wake wazalendo

kama vile Abdulghani Msoma, ilifanya vizuri mno kwa kuweza kutuletea ushindi nchini sambamba na kutoa vipaji vingi kama vile Karume Mussa, Seif Bausi, Zahor Salum, Dua Said na kadhalika.

Kwa kuwa makocha wazalendo bado wapo na bado wanaipenda nchi yao pamoja na soka kwa ujumla.

(a) Je, ni lini SMZ itaendeleza hamasa, utashi, ujenzi pamoja na mbinu za makocha wetu wazalendo kwa kuweza kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi matembezi ya kimafunzo *(study tours*) pamoja na warsha za Kimataifa

(b) Kuendelea kuwatelekeza makocha wetu wazalendo pamoja na kushindwa kuleta makocha wa kimataifa huko si kuangamiza mchezo wa mpira wa miguu ambao unapendwa na wananchi walio wengi.

Mhe. Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa ruhusa yako namba 36 nimjibu Mhe. Nassor Salim Ali.

Lakini kabla ya kumjibu napenda kumshukuru Mhe.Mwakilishi kwa kujali michango inayotolewa na makocha wa Soka Wazalendo kuweza kuibua na kukuza vipaji vya wanasoka wengi hapa nchini.

(a) Mhe. Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba serikali imekuwa ikiendeleza hamasa, utashi na ari za makocha wazalendo kwa kuwapatia mafunzo ya kuendeleza ujenzi wao kila hali inaporuhusu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, si kweli kwamba serikali imekuwa ikiangamiza mchezo wa mpira wa miguu, kuwatelekeza makocha wetu kwa kushindwa kuleta makocha wa kimataifa. Uamuzi tulionao ni kuwatumia makocha wazalendo badala ya kigeni ambao ndio wanaotuletea mafanikio.

Kwa hivyo, tunafahamu tuliponyakuwa kombe la Kagame tuliwezeshwa na kocha Mzalendo, tulipochukua kombe la vijana chini ya miaka 19 mwaka 2003 tuliwezeshwa na kocha mzalendo, na tumeshika nafasi ya tatu ya Kombe la Kagame mwaka 2012, pia tuliwezeshwa na kocha mzalendo. Tunathamani kazi zao, Baraza la taifa la Michezo kwa mashirikiano na Chama cha Mpira wa Miguu *ZFA* hapa wamekuwa wakiwaenzi na

kuwaendeleza kiujuzi na kuwaandalia mpango maalumu wa kuwapatia mafunzo makocha wetu.

Mafunzo haya yamekuwa yakifanyika Unguja na Pemba kila mwaka na kuwahusisha makocha wengi na yanaendeshwa na walimu mahiri sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni Zanzibar ilipata bahati kwa ujio wa Kocha wa Timu ya Taifa ya Italy na Kocha huyu ameonesha mapenzi makubwa kwa Zanzibar.

(a) Je, wizara kwa kushirikiana na Baraza la Michezo na *ZFA* mna mpango gani wa kutumia fursa hii ya kocha huyu wa Timu ya Taifa ya Italy ili kuwapa mafunzo makocha wetu na kuweza kupata ujuzi zaidi na kuendeleza Serikali yetu ya Zanzibar.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tulikuwa tunashiriki mashindano mbali mbali ya kimataifa kwa nchi ambazo si wanachama wa *FIFA*. Na mara nyingi tumekuwa tukishiriki katika mashindano haya na timu yetu kufanya vizuri katika mashindano haya. Lakini kwa kipindi kirefu timu yetu hii imekuwa haishiriki katika mashindano haya. Ni sababu gani zilizoifanya isiweze kushiriki katika mashindano haya ambao sie wanachama wa *FIFA*.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Italy ni kweli kwamba mwaka jana mwezi wa Oktoba, Novemba na Disemba na hata Januari tulikuwa naye huyu alikuja mwanzoni na tukafanya mazungumzo naye makubwa, halafu tunamshukuru tulimualika na akaja tena tumekuwa naye na tumekaa pamoja na Baraza la Michezo wakakaa pamoja na *ZFA* wameandaa mpango maalumu endelevu wa kuhakikisha kwamba wanashirikiana na *ZFA* pamoja na Chama cha Soka cha Zanzibar, kuona namna gani watafanya utaratibu wa kuibua vipaji na pia kuunda timu za Taifa si moja nyingi ili hatimaye tuwe na Timu ya Taifa moja kubwa ambayo itakuwa ndiyo msingi wa Timu yetu ya Taifa kushiriki katika mashindano ya kimataifa.

(b) Kwa taarifa tuliyokuwa nayo ni kwamba mashindano haya ya nchi ambazo si wanachama wa *FIFA* ni kwamba umoja wenyewe umekuwa kidogo hauko imara umekuwa ukibadilika badilika kila mara. Sasa *ZFA* na Baraza la Michezo inaona kwanza iangalie uongozi kwanza Umoja huu wa

Vyama ambavyo si wanachama wa *FIFA* wa nchi hizi. Halafu ndio baadae tuweke mikakati mizuri ya kushiriki. Kwa hiyo pale tutakapoona sasa tumeshakuwa na chama ambacho ni madhubuti kwa nchi hizi hapo *ZFA* itashiriki katika michezo hii na hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania linapata msaada wa fedha kwa ajili ya kuendeleza makocha Tanzania, lakini kuna taarifa kwamba zinatumika kwa chama cha Mpira wa Miguu Tanzania *TFF*.

(a) Je, kwa nini Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar hakipati fedha hizo.

(b) Ni mikakati gani ifanyike ili Zanzibar nao wapate fedha hizi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba *TFF* imekuwa ikipata fedha kutoka *FIFA* na *ZFA* imekuwa haipati fedha hizi. Tatizo kubwa ni kwamba *TFF* ndie Mwanachama wa *FIFA* na *ZFA* si mwanachama wa *FIFA*. Sasa *TFF* wakishapata fedha kutoka *FIFA* tunatumia kwa ajili ya kushughulikia timu ambazo wanasimamia za Tanzania Bara sio za Zanzibar. Hii ni kwa sababu ya mfumo tulionao wa Muungano wetu Mhe. Mwenyekiti. Tufanyeje?

Mhe. Mwenyekiti, tunaenda katika Bunge la Katiba, kwa hiyo ni juu yetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuamua mfumo upi ambao utaiwezesha Zanzibar kupata fursa katika Mashirika ya Kimataifa. Kwa hivyo, hili ndilo jambo lilioko sasa hivi.(*Makofi*).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mwaka 1974 Timu ya Simba tukiongozwa na Timu Kampeni Haidar Abeid Michacho na golikipa Othman Mambosasa chini ya Kocha mzalendo tuliweza kufanya vizuri sana mwaka 1974 tulipowaadhirisha Accra pale Ghana kwao na kuweza kuingia nusu fainali chini ya Kocha Paul Gwivaa Mzalendo.

Sasa wenzetu Bara wanawapatia *course* za muda mrefu na muda mfupi za nje ili kuangalia uzoefu wa nchi nyengine katika masuala ya soka.

(a) Je, ni lini Tanzania itatumia Makocha wetu wazalendo wakiwemo vijana ambao walicheza soka sana hapa akina Abdulwakati Juma, Fueni Ali ambao sasa hivi wako pale Oman. Wakawapatia *course* za nje ili wakija hapa wewe makocha vilabu vyetu viwe vizuri kama tulivyofanya sisi Simba mwaka 1974.

(b) Wenzetu wameanzisha *program* kule Bara kadhaa ambazo, *program* hizi zinafanya timu zao ziwe nzuri kwa mfano wameanzisha *Airtel Rise Star*. Ni lini Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar itazishajihisha hizi kampuni kubwa kwa mfano hii Kampuni ya *Azam Marine*, *Zantel* na wao waanzishe ili na sisi tuweze kuwa na zetu hapa nchini.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kumjibu muasisi Mhe. Saleh Nassor Juma mwanamichezo maarufu sana katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, ndani ya Baraza la Wawakilishi kuna wanamichezo wa aina mbili; kuna wa michezo wa ndani ya Baraza la Wawakilishi na kuna wanamichezo wa ndani ya viwanja vya michezo.

Kwa hivyo, Mhe. Saleh Nassor Juma ni mmoja katika mwanamichezo mzuri sana katika Baraza la Wawakilishi nampongeza sana kwa hilo.

(a) Suala la lini Zanzibar sio Tanzania kwa sababu mimi nasimamia michezo hapa Zanzibar. Lini Zanzibar itaandaa *program* mbali mbali za mafunzo katika kuwaandaa makocha wetu. Mhe. Mwenyekiti, hili tumelianza hivi sasa hata mwaka jana tulikuwa na makocha 40 wa Zanzibar walipata mafunzo yalikuwa yakisimamiwa na walimu kutoka Uingereza hapa Zanzibar. Kwa hivyo, uone kwamba jitihada hizi tumezianzisha zinaendelea na pamoja na hayo kila Jumamosi na Jumapili katika Skuli ya Haile Selassie walimu waliopata mafunzo nje ya Zanzibar wanawafundisha wenzao makocha wa hapa Zanzibar.

Na kwa kweli mafunzo haya yamepata heshima kubwa na wameweza kuinua kiwango cha makocha wetu. Tuna makocha kiasi 12 ambao wana *class B.* Hii ni kwa sababu ya suala hili.

(b) Kuhusu suala la kushajihisha wafanyabiashara na makampuni mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, ushauri huo tunauchukua na tutakwenda kuufanyia kazi na tutamjibu mwanamichezo Mhe. Saleh Nassor Juma wapi tumefikia katika hili.

Nam. 48

Huduma ya Maji kwa Wasiopata Huduma hiyo kwa Uhakika

Mhe. Asha Abdu Haji: Aliuliza:-

Kwanza kabisa naipongeza Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa huduma zake nzuri za kuwahudumia watu wote wa Zanzibar, wanapata maji safi na salama licha ya matatizo makubwa inayoyapata katika juhudi zake za kutimiza lengo lake la kuwapatia maji watu wote.

(a) Je, kwa nini wizara inawataka watu wasiopata maji kulipia malipo ya kila mwezi kwa sababu tu ndani ya nyumba zao mna mifereji

(b) Kwa nini wizara haifanyi uchunguzi wa kina na kuzitaka nyumba zinazopata maji kulipia na kuziacha zile zisizopata maji huku ikiendelea kutafuta ufumbuzi wa tatizo la kutopatikana maji kwa nyumba hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Asha Abdu Haji swali lake namba 48 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutokubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu inawataka watu wasiopata huduma ya maji kulipia malipo ya mwezi kwa sababu tu ndani ya nyumba zao mna mifereji.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi napenda kutoa ufafanuzi mbele ya Baraza lako tukufu kwamba suala la kulipia huduma ya maji ni la kisheria ambayo inamtaka kila mwananchi anayepata huduma ya maji safi na salama kulipia huduma hiyo bila ya kujali Mkoa, Wilaya ama Shehia anayoishi. Kinachoangaliwa ni upatikanaji wa huduma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka ya maji inaendelea na zoezi la kuzitambua nyumba ambazo hazipati huduma hiyo na kufanya jitihada na kuhakikisha kwamba huduma hiyo inapatikana ndani ya maeneo yote ya Mjini Magharibi pamoja na maeneo ya vijijini.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa serikali ilijitahidi kuwawekea mifereji wananchi ambao hawana uwezo wa kuingiza mifereji hiyo ndani, na kwa kuwa juzi tu *ZAWA* walienda Jambiani na kuikata mifereji ya nje baadhi. Je, ni kweli serikali ina huruma na walipa kodi wake ambao hawana uwezo wa kuingiza mifereji ile ndani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji *ZAWA* mara zote inaposambaza miundombinu ya maji basi ina utaratibu wa kuweka mifereji ya nje kwa makusudi ya kuwawekea wale wananchi wanyonge ambao hawana uwezo wa kuingiza ndani mifereji hiyo. Lakini baada tu ya mamlaka kufanya hivyo hujitokeza baadhi ya mafundi wasiokuwa rasmi na kuongezea mifereji mingine isiyotambulikana kisheria.

Kwa hiyo, inapogundulikana mifereji ya aina hiyo Mamlaka ya Maji huchukua jitihada ya kuing'oa ile mifereji ambayo haikuwekwa kisheria na Mamlaka ya Maji.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nichukue fursa hii kukushukuruni sana kwa namna tulivyoshirikiana kwa pamoja toka mwanzo wa shughuli zetu kwa siku ya leo hadi kufikia hapa.

Kwa taarifa tu ambayo tayari tumeipokea kutoka kwa Katibu shughuli zetu za Baraza hili zinaishia hapa kwa sasa hivi. Na kwa sasa basi nachukua fursa hii kuakhirisha Baraza hili hadi saa 11:00 jioni wakati ambapo Makamu wa Pili wa Rais atatoa hotuba ya kufunga Baraza hili.

Kwa maelekezo hayo naomba kuakhirisha Baraza hili hadi jioni saa 11:00 kwa Wajumbe wote kuwemo humu ndani. Ahsanteni.

(Saa 4:55 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili kutoa hotuba ya kutufungia shughuli zetu, baada ya kumaliza shughuli zote ambazo zilikuwa zimepangwa kwa ajili ya mkutano huu nataka nitoe taarifa. Waheshimiwa Wajumbe kama mtakavyokumbuka katika kikao cha tano cha mkutano huu ambao tunategemea kuumaliza leo hivi punde, siku ya Jumanne tarehe 28 Januari mwaka huu, Baraza liliamua tuunde Kamati Teule kuchunguza kadhia iliyotokezea katika Nyumba yetu ya Nyaraka ambayo ni hazina muhimu ya kumbukumbu zetu kwa ajili ya nchi yetu ya Zanzibar.

Baada ya maamuzi hayo nilikaa na kuzingatia na kama kanuni inavyohitaji chini ya kanuni 120 kifungu kidogo cha 3 cha kanuni hiyo, ambapo Spika anategemewa baada ya maamuzi ya Baraza kuteua na kuitangaza hiyo Kamati

Teule. Naomba Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii sasa kutangaza hiyo Kamati Teule kama kifungu hicho kinavyonitaka nifanye hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe Kamati Teule yetu itakuwa na Wajumbe watano ambao watafanya kazi ya kuchunguza suala zima la upotevu wa nyaraka katika Nyumba yetu ya Nyaraka Kilimani. Lakini vile vile kuchunguza na hatimae kupendekeza njia mbali mbali muafaka ambazo nyaraka zetu nyengine zitakuwa salama. Na jambo la aina hiyo la upotevu wa nyaraka muhimu kwa kiasi kikubwa hautatokezea tena, ili kuhakikisha kwamba hazina yetu ya nyaraka inakuwa salama, ya kudumu kwa ajili ya vizazi vya kesho na siku nyingi zijazo. Pia kwa ajili ya rejea kwa wageni wetu mbali mbali wanaokuja na kufikia katika nyumba yetu ile ya nyaraka, ili kujua mambo yaliyotokezea huko nyuma na hali halisi ya namna kumbukumbu zetu ambavyo tunazihifadhi kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Kamati yenyewe ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ussi Jecha Simai
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
3. Mhe. Ashura Sharif Ali
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid

Wajumbe hawa watano Waheshimiwa Wajumbe, ndio ambao wataunda Kamati hiyo Teule na tunategemea ifanye kazi katika kipindi cha siku saba katika wakati muafaka kufuatana na wasaa utakavyokuwa, hasa hasa mbele ya shughuli muhimu ambayo iko mbele yetu, ambayo rasmi hatujajua itaanza lini.

Kwa hiyo Katibu atakuwa anawasiliana na Wajumbe hao mapema iwezekanavyo, ili Waheshimiwa Wajumbe wajue tarehe halisi ya kuanza shughuli hiyo ya kuchunguza suala zima la upotevu wa nyaraka zetu katika Nyumba ya Nyaraka hapo Kilimani.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya maelezo hayo, naomba nikushukuruni kwa kunisikiliza. Na pia kwa mashirikiano makubwa ambayo mmekuwa nayo kwa muda wote wa vikao vyetu. Na sasa ni wakati muafaka nimuombe na nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili aweze kufanya kazi iliyobaki na hatimae kutufungia mkutano wetu huu.

KUAHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu na mwingi wa rehma, kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutupa nguvu za kuweza kutimiza majukumu yetu yote tuliyojipangia katika kipindi hiki kwa salama na amani.

Pili, nakushukuru wewe Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wako kwa kuuongoza Mkutano wa 15 wa Baraza letu kwa umakini, busara na hekima kubwa. Nawashukuru Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi kwa msaada mkubwa waliokupa katika kuliendesha Baraza hili tukufu kwa mafanikio makubwa na kumaliza shughuli zake salama.

Mhe. Spika, pia nawashukuru kwa dhati Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza kwa kuziongoza Kamati zao na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake imara ambao unaendelea kutupatia mafanikio makubwa ya kimaendeleo katika nchi yetu katika nyanja zote. Ushauri, maelekezo na miongozo yake inatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi.

Uchaguzi wa Jimbo la Kiembesamaki

Mhe. Spika, tarehe 2 Februari, 2014 wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki walifanya uchaguzi na kupata Mwakilishi wao ambae anatokana na ridhaa ya wananchi wa Jimbo hilo. Katika uchaguzi huo Mhe. Mahmoud Thabit Kombo aliyegombea kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi aliibuka na ushindi mnono na kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki.

Mhe. Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa ushindi mnono alioupata kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kuwa Mwakilishi wao. Wananchi wa Jimbo hilo wamefanya uamuzi wa busara wa kumchagua Mhe. Mahmoud Thabit Kombo. Hongera sana Mhe. Mahmoud Thabit Kombo. *(Makofi)*

Wewe sio mgeni wa Baraza hili ingawa ni mgeni wa ukumbi huu. Umekuwemo katika Baraza la Wawakilishi miaka kadhaa iliyopita na tunaikumbuka michango yako uliyokuwa unaitoa ukiwa Mwakilishi wa Jimbo

la Mpendae na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Ni matumaini yetu kwamba Baraza hili litafaidika tena na michango yako katika kipindi hiki.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii pia kuwapongeza wagombea wote pamoja na vyama vyao kwa kushiriki vyema katika uchaguzi huo ambao ulikuwa huru na wa haki na ulifanyika kwa salama, amani na utulivu mkubwa. Uchaguzi huo umekwisha na sasa ni wakati wa kushirikiana kwa pamoja katika kuendelea kuiletea maendeleo nchi yetu. Aidha, niwapongeze wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kwa kushiriki kwa wingi na kwa amani katika uchaguzi huu.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumpa pole nyingi Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma ambaye kwa sasa yuko matibabuni Afrika Kusini na kumuombea Mungu ampe nafuu haraka ili aje kuungana nasi katika ujenzi wa nchi yetu.

Narudia tena kuwahakikishia wananchi na Baraza lako tukufu kwamba Mhe. Maalim Haroun yuko salama na hali ya afya yake inazidi kuimarika. Ni jana tu nilizungumza na mwanawe Ali ambaye amenihakikishia kuwa hali ya Maalim Haroun alikuwa anaendelea vizuri na kwa mujibu wa maelezo ya Daktari wake huenda akaruhusiwa kurudi nyumbani mnamo mwanzoni mwa mwezi ujao.

Mhe. Spika, napenda pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kujadili kwa kina miswada na ripoti mbali mbali ambazo ziliwasilishwa kwenye Mkutano huu wa Kumi na Tano. Ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wajumbe kupitia mijadala hiyo utasaidia sana katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Vile vile, niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kujibu vizuri maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe na pia kutoa ufafanuzi wa kina kwa hoja mbali mbali zilizoibuka kwenye Mkutano huu.

Mambo yaliyojitokeza nchini

Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar

Mhe. Spika, tarehe 12 Januari, 2014 ilikuwa ni siku ya kilele cha Maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kutimiza miaka 50, maadhimisho ambayo yalizinduliwa rasmi tarehe 15 Agosti, 2013

na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein.

Katika kipindi chote cha maadhimisho ya sherehe hizo tulishuhudia kufanyika mambo mbali mbali, ikiwemo uwekaji wa mawe ya msingi na ufunguzi wa miradi mbali mbali ya maendeleo, kulikuwa na matamasha mbali mbali ya michezo na muziki, maonesho na fensi, warsha na makongamano yaliyowashirikisha wananchi wengi. Jumla ya miradi 73 ilifunguliwa na miradi 41 iliwekewa mawe ya msingi.

Aidha, siku ya kilele tulishuhudia gwaride na maonesho ya kijeshi ya aina yake yaliyoandaliwa na Vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama, maandamano ya wananchi wa Mikoa yote mitano ya Zanzibar na halaiki ya vijana wetu iliyopendeza sana.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na wananchi wote kwa jumla kwa kushiriki kikamilifu katika matukio mbali mbali wakati wa shamra shamra za miaka 50 ya Mapinduzi yetu. Pia, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Viongozi wote waliokuwa wageni rasmi katika matukio mbali mbali.

Aidha, naishukuru sana Halmashauri ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na Kamati zake zote kwa kazi kubwa waliyoifanya hadi kufanikisha sherehe zetu ambazo zilikuwa za aina ya kipekee. Niwashukuru pia Vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama, wanafunzi wa halaiki, wasanii, wanahabari na wananchi wote ambao walishiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha maadhimisho haya.

Hali ya Amani, Utulivu na Usalama Nchini

Mhe. Spika, amani, utulivu na usalama katika nchi ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya nchi yoyote duniani. Tanzania ni nchi inayoendelea kuheshimika katika Bara la Afrika na duniani kwa jumla kwa jinsi tunavyodumisha amani, utulivu na umoja katika nchi yetu. Hivyo, ni vyema kila mmoja wetu kuilinda na kuidumisha hali hii, ingawa katika siku za hivi karibuni kumejitokeza vikundi vya watu wachache wanaowasumbua wananchi kwa kuwavamia katika nyumba zao, kupora mali na kuwahatarishia maisha yao. Serikali haitavumilia kuona vitendo hivi vya uvunjifu wa amani vikifanyika katika nchi hii.

Naliagiza Jeshi la Polisi kufanya kila linalowezekana kuwasaka na kuwakamata wote wanaohusika na vitendo hivyo na kuwafikisha katika vyombo vya sheria. Aidha, tunawaomba wananchi kuimarisha hali ya ulinzi katika maeneo yao na kutoa taarifa kwa vyombo husika mara moja wakigundua kuwepo dalili za uvunjifu wa amani na usalama katika maeneo yao. Tunataka wananchi wetu wafanye shughuli zao za kuendesha maisha yao na ya familia zao kwa njia ya amani na utulivu bila ya kuwa na hofu yoyote.

Ununuzi na Uuzaji wa Zao la Karafuu

Mhe. Spika, karafuu ni zao muhimu katika uchumi wa nchi yetu na huchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa na kuinua maisha ya wananchi wetu. Katika msimu wa karafuu wa mwaka 2013/2014, Serikali hadi kufikia tarehe 27 Januari, 2014 imeshanunua jumla ya tani 4995.4 za karafuu zenye thamani ya T.Shs. 69.89 bilioni. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 119 ya lengo la kununua tani 4,200 kwa msimu wa mwaka huu. Aidha, Serikali tayari imeshauza karafuu nje ya nchi jumla ya tani 4,272 kwa thamani ya T.Shs. 73.03 bilioni.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wa zao la karafuu nchini mwetu, Serikali imefanya jitihada za kuwainua wazalishaji wa zao hili kwa kutoa bei nzuri ya ununuzi wa karafuu zetu. Aidha, Serikali imewashajiisha wakulima wa karafuu kwa kuwapatia miche ya mikarafuu bure ili waweze kuotesha mikarafuu mingine mipya katika mashamba yao itakayozaa vizuri, tofauti na ile ya zamani ambayo kwa sasa mingi yao imechoka na kiwango cha uzalishaji ni mdogo.

Mhe. Spika, huku Serikali ikifanya jitihada hizo kwa lengo la kuzalisha karafuu zaidi, kumeibuka watu wachache miongoni mwetu ambao hupita kwenye maeneo mbali mbali, kuwarubuni wakulima na kununua karafuu zao na baadae kuzisafirisha kwa njia za magendo na kwenda kuziuza nje ya nchi yetu. Watu hawa pia huwaibia wananchi kwa kutumia vipimo visivyo sahihi kwa ajili ya kujipatia manufaa zaidi. Watu wa aina hii ni wahalifu na ni wahujumu wa uchumi wetu.

Natoa wito kwa wananchi kuwa macho na watu hawa na wasiwauzie karafuu zao wababaishaji wanaopita majumbani mwao, na yeyote ambae atafanya hivyo pelekeni taarifa mara moja kwa viongozi wenu wa Shehia au Jeshi la Polisi ili waweze kuchukuliwa hatua zinazofaa. Serikali imeweka Taasisi Maalum ya kununua na kuuza karafuu zetu ambayo ni *ZSTC* pekee, chombo

ambacho kimeendelea kutekeleza majukumu yake kwa umakini na kutoa huduma bora zaidi za soko kwa wakulima wa zao la karafuu.

Aidha, nakipongeza sana Kikosi chetu cha KMKM kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kuwakamata wanaofanya biashara ya magendo. Nawapongeza raia wema wote wanaotoa taarifa kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama wanapobaini kuwepo kwa vitendo hivyo viovu, vyenye nia ya kuinyima Serikali mapato yake

Mwenendo wa Bei za Bidhaa

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2013 kumekuwa na utulivu wa bei za bidhaa kama vile mchele, sukari na unga wa ngano jambo ambalo linaleta faraja sana kwa wananchi wetu. Serikali inawapongeza sana wafanyabiashara wetu na inawataka waendelee kushirikiana na Serikali kwa kujadiliana na kushauriana masuala mbali mbali ya bei za bidhaa hasa mchele, sukari na unga wa ngano kwa lengo la kuwapunguzia wananchi wetu ukali wa maisha. Serikali inawaomba wafanyabiashara kuendelea kuagiza bidhaa hizo kwa wingi na kuuza kwa bei ambazo wananchi wanaweza kununua.

Usambazaji wa Huduma za Mkonga wa Mawasiliano

Mhe. Spika, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya *Zantel* inaendelea na kazi ya kusimamia usambazaji wa Mkonga katika Taasisi za Serikali Unguja na Pemba. Hadi sasa zaidi ya taasisi 80 za Serikali tayari zimeshasogezewa Mkonga wa Mawasiliano na kufungwa kifaa maalum cha kusambazia huduma hiyo *(Optical Distribution Frame).* Serikali inaziomba taasisi zake zote kukamilisha uwekaji wa mtandao wa ndani *(LAN)* kwenye majengo yao ili waweze kufaidika na huduma za mtandao kupitia Mkonga huo.

Tatizo la Dawa za Kulevya

Mhe. Spika, suala la uingizaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya bado linaendelea kuwa tatizo katika nchi yetu. Tatizo hili linatishia afya na maisha ya watu wetu, na hasa vijana na hivyo kuhatarisha uimara wa uchumi na maendeleo ya Taifa letu. Tukio la hivi karibuni la kukamatwa mabegi mawili yenye ujazo wa jumla ya kilo 30 za dawa za kulevya katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ni la kusikitisha sana na kuifedhehesha nchi yetu. Serikali itawasaka kwa nguvu zote wale wote waliohusika na dawa zilizokamatwa na kufikishwa katika vyombo vya Sheria na mtandao wao wa udhalimu huu kudhibitiwa.

Mhe. Spika, Serikali itaendelea na juhudi zake za kupambana na wale wote wanaojihusisha na biashara hii haramu bila ya kujali nyadhifa zao, umaarufu wao na hali zao za maisha. Aidha, Serikali itaendelea kuelimisha jamii juu ya madhara ya utumiaji wa dawa hizi hatari kwa maisha ya binadamu. Naomba kuwasihi wale wote wanaohusika na udhibiti wa uingiaji na usambazaji wa dawa za kulevya kuwa makini na utendaji wao wa kazi kwani kuanzia sasa Serikali itachukua hatua kali kwa watakaobainika kushiriki kwa namna yeyote katika biashara hii haramu.

Hata hivyo, vita hivyo sio vya Serikali peke yake, bali ni vyetu sisi sote wananchi. Wananchi wakitimiza wajibu wao wa kuwafichua wanaohusika na biashara hii, vita hivi vitakuwa rahisi kushinda.

Vyombo vya Usafiri wa Baharini

Mhe. Spika, mnamo tarehe 5 Januari, 2014 kulitokea ajali katika maeneo ya Nungwi wakati meli ya MV Kilimanjaro II ilipokuwa ikitoka Pemba kuelekea Unguja. Ajali hiyo ilisababishwa na upepo mkali na Nahodha alishindwa kuihimili boti na baadhi ya abiria waliokuwa wamekaa juu na pembezoni mwa meli hiyo walianguka na kutumbukia baharini. Serikali imeunda Tume ya Uchunguzi ili kujua chanzo na sababu za kutokea ajali hiyo na taarifa ya uchunguzi huo itatolewa kwa wananchi mara tu Tume hiyo itakapokamilisha na kuwasilisha ripoti yake.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuwapa mkono wa pole ndugu na jamaa wote ambao walipoteza ndugu zao kwenye ajali hiyo. Mungu awape moyo wa subira na uvumilivu, amin. Pia nawapa pole wale wote ambao kwa njia moja ama nyengine waliathirika na ajali hiyo. Mungu aendelee kuwapa afya njema.

Mhe. Spika, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa yanayoendelea kuikumba dunia na katika sehemu za nchi yetu, ni muhimu kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri baharini, manahodha na wananchi kwa jumla kufuatilia maelekezo yanayotolewa na taasisi husika kuhusu mwenendo wa hali ya hewa, na kuchukua hadhari wakati wanaposafiri kwa kutumia vyombo vya baharini.

Aidha, napenda kutoa pole nyingi na za dhati kwa wananchi wa Micheweni kwa maafa waliyoyapata ya kuunguliwa na nyumba zao. Mimi mwenyewe nilikitembelea kijiji kilichoathirika na maafa hayo na kuiona hasara kubwa iliyopatikana. Ninawaomba wananchi wa Micheweni wawasaidie wenzao walioathirika ili waweze kurejea katika hali zao za kawaida. Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuwasaidia wananchi hao kadri itakavyoweza.

Bunge la Katiba

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba nchi yetu imo kwenye hatua za kupata Katiba Mpya na tayari Tume ya Mabadiliko ya Katiba chini ya Mwenyekiti wake Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba imeshakabidhi Rasimu ya Pili ya Katiba hiyo kwa Serikali zote mbili. Hatua iliopo mbele yetu sasa ni kuwa na Bunge la Katiba litakalojadili na kupitisha Rasimu ya Katiba Mpya na baadae kupigiwa kura ya maoni na wananchi.

Watendaji wetu wa Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana na watendaji wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanaendelea kuandaa kanuni pamoja na taratibu nyengine zitakazoongoza Bunge hilo linalotarajiwa kuanza hivi karibuni baada ya majina 201 ya Wajumbe watakaoingia katika Bunge hilo kutangazwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mnamo siku chache zijazo. Taratibu zote zitakapokamilika Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na Wajumbe wengine wa Bunge hilo watajulishwa rasmi.

Tunawaomba Waheshimiwa wote watakaobahatika kushiriki katika Bunge hilo kutilia maanani maslahi ya nchi yetu, umoja na mshikamano wetu na uhai wa Taifa letu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina mwongozo wa kutoa kwa washiriki wa Zanzibar ili kumfanya kila mshiriki awe huru kuichambua na kuijadili rasimu hiyo kadri atakavyoona inafaa. Mwisho wa yote tungependa kuona nchi inapata Katiba Mpya itakayokuwa nzuri na yenye maslahi kwa wote.

Migogoro ya Ardhi

Mhe. Spika, tangu Awamu ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuingia madarakani suala la kutatua migogoro ya ardhi limepewa kipaumbele kwa kufanya juhudi mbali mbali.

Kama hatua ya msingi tumeanza na mapitio ya Sera ya Ardhi kwa vile sera ndio dira kuu ya kusimamia na kuendeleza matumizi bora na endelevu ya ardhi. Sera hiyo itakapokamilika ndio itakayotoa miongozo ya muda mfupi na ya muda mrefu juu ya mustakbali mzima wa ardhi, na kuondoa mianya ya uwezekano wa kutokea migogoro ya ardhi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kuendeleza jitihada za kupatia ufumbuzi wa kudumu migogoro yote ya ardhi, Serikali imechukua jitihada zifuatazo:-

Mahakama za Ardhi

Mahakama za Ardhi zimeimarishwa kwa kuongezwa idadi ya Mahakama katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba sambamba na uteuzi wa Mahakimu katika Mahakama hizo. Aidha, idadi ya Wazee wa Baraza imeongezwa ili kuharakisha maamuzi ya utatuzi wa migogoro ya ardhi. Uimarishaji huo wa Mahakama umeleta matokeo mazuri. Kwa mfano, katika kipindi cha miezi sita (6) iliyopita jumla ya kesi 187 zimeweza kutolewa maamuzi.

Kufanywa Marekebisho ya Sheria ya Umiliki wa Ardhi Nam. 12 ya 1992

Mnamo mwaka 2013, Baraza la Wawakilishi lilipitisha marekebisho madogo madogo *(Miscellaneous Ammendments)* ya sheria ambayo yatarahisisha ulipaji wa fidia pindipo Serikali inapolichukua eneo la mwananchi kwa manufaa ya Taifa.

Usajili wa Ardhi

Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati inaendelea na kazi ya kumtambua na kumthibitisha kila mwenye haki ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba kwa lengo la kuondoa migogoro ya ardhi. Utambuzi ni hatua ya awali katika kufikia lengo kuu la kusajili asilimia hamsini ya ardhi yote ya Zanzibar ifikapo mwaka 2015.

Uhaulishaji wa Ardhi

Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imepata mafanikio makubwa ya utendaji wa kazi za uhaulishaji wa ardhi kwa kuondoa athari za kutapeliwa na kudhulumiwa kutokana na umakini katika utendaji kazi wa Bodi ya Uhaulishaji.

Kuchukua hatua za nidhamu

Serikali imechukua hatua mbali mbali za kinidhamu kwa watendaji wote wanaobainika kwa namna moja au nyengine ni chanzo cha migogoro ya ardhi na uvunjaji wa sheria za ardhi.

Utaratibu wa upimaji na ugawaji wa ardhi

Mhe. Spika**,** Serikali kupitia Wizara husika imeanzisha mfumo wa kuwashirikisha Viongozi wa Mikoa, Wilaya, Masheha na Madiwani katika taratibu zote za upangaji na upimaji wa ardhi. Aidha, mpango mkuuu wa matumizi ya ardhi Zanzibar *(National Land Use Plan)* kwa mara ya kwanza umeshirikisha wadau wote waliotajwa hapo juu, ili kila mdau aweze kujiona kama ni mshiriki kamili wa maendeleo ya eneo lake na mlinzi dhidi ya ujenzi holela.

Pia, ningependa kutoa wito kwa wananchi kushiriki kikamilifu kwenye zoezi la usajili wa ardhi ambalo kwa sasa linagharamiwa na mradi wa *Smole* na mpango wa MKURABITA. Hivyo, ni vyema wananchi waitumie kikamilifu fursa hii adimu na adhimu.

Mambo yaliyojitokeza Barazani

Mhe. Spika**,** katika Mkutano huu wa Kumi na Tano jumla ya maswali 40 ya msingi na maswali 92 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na kupatiwa majibu na ufafanuzi na Waheshimiwa Mawaziri. Pia, Waheshimiwa Wajumbe walijadili na kupitisha Miswada miwili:-

1. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

2. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya mwaka 1985 na Kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Maelezo ya Miswada iliyowasilishwa

Mhe. Spika, Mswada wa Kwanza ambao uliwasilishwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kupata nafasi ya kuujadili ni Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Madhumuni ya Mswada huu ni pamoja na kuweka mfumo utakaowatambua na kuwalinda wagunduzi wa aina mpya ya mbegu za mimea waliopo na watakaokuja nchini na kulinda hakimiliki zao.

Pia, Mswada huu una lengo la kuongeza na kuvutia uwekezaji kwenye sekta ya kilimo kwa kuongeza hamasa katika ugunduzi wa mbegu mpya zinazokidhi mahitaji ya wakulima na masoko pamoja na upatikanaji wa taarifa muhimu ikiwa ni pamoja na matokeo ya majaribio ya kitaalamu na upatikanaji wa teknolojia mpya za utafiti na ugunduzi wa mbegu mpya.

Aidha, kupatikana kwa Sheria hii hapa Zanzibar kutaiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza masharti ya kujiunga na Shirika la Kimataifa la Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea *(International Union for the Protection of New Varietees of Plants – UPOV)*. Kwa kujiunga na Shirika hilo, Tanzania itapata faida nyingi zinazohusiana na masuala ya maendeleo ya kilimo.

Mhe. Spika**,** Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya mwaka 1985 na Kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo nao uliwasilishwa ndani ya Baraza lako Tukufu na kujadiliwa na Waheshimiwa Wajumbe. Mswada huu umeanzishwa kutokana na mapungufu mengi yaliyokuwemo kwenye Sheria ya Karafuu ya mwaka 1985. Sheria hii mpya pamoja na mambo mengine pia itahusisha masuala yote yanayohusu karafuu kama vile ukulima wa zao la karafuu, uvunaji, uanikaji, uhifadhi wa mikarafuu na maeneo ya maendeleo ya mikarafuu.

Mhe. Spika, aidha, Sheria hii itaanzisha Mfuko Maalum wa Maendeleo ya Karafuu kwa lengo la kuliendeleza zao la karafuu na kuwaendeleza wakulima wa zao hilo kifedha. Vile vile, Mfuko una lengo la kusaidia uendeshaji wa tafiti kwa ajili ya maendeleo ya karafuu na kusaidia huduma za matibabu kwa wakulima na watu watakaopata madhara wakati wa shughuli za uchumaji wa karafuu. Kwa ujumla Mswada huu ni mzuri kwani utasaidia sana masuala mbali mbali ya maendeleo ya zao letu la karafuu kuhusu ukulima bora, utunzaji na uuzaji wake.

Mhe. Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kuzikubali na kuzipitisha Sheria hizi muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Naziagiza taasisi husika mara baada ya kukamilika kwa taratibu za kuanzisha Sheria hizi, kuchukua hatua za makusudi za kuielimisha jamii kuhusiana na matakwa ya Sheria hizi ili kurahisisha utekelezaji wake.

Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi

Mhe. Spika**,** katika Mkutano huu pia, Waheshimiwa Mawaziri waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa maagizo ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2012/2013. Aidha, Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza lako Tukufu waliwasilisha taarifa za Kamati zao kwa mwaka 2013/2014. Kutokana na taarifa hizo, Waheshimiwa Wajumbe walipata nafasi ya kujadili, kuibua hoja mbali mbali za msingi pamoja na kutoa ushauri utakaosaidia kuimarisha utendaji kazi wa Serikali.

Serikali itaendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na kuzifanyia kazi hoja za msingi zinazoibuliwa na Wajumbe. Dhamira ya Serikali ni kuwa na uwajibikaji utakaoleta ufanisi, tija na maslahi kwa Taifa letu. Napenda kuliahidi Baraza lako Tukufu kwamba maagizo na maelekezo yote yaliyotolewa katika Ripoti za Kamati kwa mwaka 2013/14 yatafanyiwa kazi na Serikali kwa ukamilifu.

Nawapongeza sana Mhe. Spika**,** Wajumbe wa Baraza hili namna walivyokuwa makini katika kutekeleza wajibu wao wa kuisimamia Serikali na kuibua ubadhirifu wa mali na fedha za umma unaofanywa Serikalini. Serikali itafanya kila juhudi kuirekebisha hali hiyo.

Mhe. Spika**,** nachukua fursa hii kuzipongeza Kamati zote za Kudumu za Baraza hili kwa kazi wanazozifanya za kuisaidia Serikali yetu kuimarisha utendaji na uwajibikaji. Naomba tuendelee kushirikiana katika kuiletea maendeleo nchi yetu kwa faida yetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa Serikali haidharau na wala haitodharau maagizo yanayotolewa na Kamati za Kudumu ila maagizo yote hufanyiwa kazi kikamilifu na kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa ubadhirifu huo haufanyiki na itaendelea kufanya hivyo. Serikali haitamvumilia yeyote atakaye thibitika kufanya ubadhirifu huo.

Mhe. Spika, Serikali imesikitishwa sana na taarifa za upotevu wa nyaraka za serikali kutoka katika nyumba inayoshughulikia utunzaji wa nyaraka za serikali na mambo ya kale. Serikali imekubaliana na uamuzi wa Baraza wa kuunda Kamati Teule ili ukweli wa wahusika wa kitendo hiki ujulikane.

Ni matarajio yangu kwamba kamati itafanya kazi zake haraka iwezekanavyo kama ilivyoagizwa na Mhe. Spika.

Uwasilishaji wa Bajeti ya Serikali na bajeti za Mawizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015

Mhe. Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Serikali inakusudia kubadilisha mfumo wa kuwasilisha Barazani mapendekezo ya bajeti kuwa katikati au mwishoni mwa mwezi wa Mei badala ya mwezi wa Juni. Kwa mwaka ujao wa fedha (2014/2015) bajeti itawasilishwa katika mwezi wa Mei na kumalizika mwishoni mwa mwezi wa Juni kabla ya kuanza Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Hivyo, ni vyema kwa Mawizara kuanza maandalizi ya mapema ya hotuba zao za bajeti na pia Kamati za Baraza na Wajumbe wa Baraza kujipanga kuendana na mabadiliko hayo.

Hitimisho

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nichukue nafasi hii kukupongeza tena wewe binafsi, wasaidizi wako pamoja na watendaji wote wa Baraza kwa kutekeleza majukumu yenu kwa uadilifu na ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika**,** pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kwa ushauri wao wenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa Majukumu ya Serikali. Ni imani yangu kwamba, Waheshimiwa Wawakilishi wanapoibua hoja mbali mbali ndani ya Baraza hili wana lengo la kuisaidia Serikali yetu ili iwe makini zaidi katika utendaji kazi wake.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niwashukuru waandishi wa habari, wakalimani wa alama kwa kazi zao nzuri za kuipasha habari jamii. Nawashukuru wananchi wote kwa kufuatilia mijadala ya Baraza kupitia vyombo vyetu vya habari na kuendelea kuiamini serikali yao na kudumisha amani, utulivu na mshikamano katika nchi yetu.

Mhe. Spika**,** nawatakia Waheshimiwa Wawakilishi wote kurudi vituoni mwao salama kwenda kuwahudumia wananchi Majimboni mwao.

Mhe. Spika**,** baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako Tukufu hadi tarehe 14 Mei, 2014, Saa 3 kamili za asubuhi.

Mhe. Spika**,** naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kwa niaba yenu nimshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba nzuri, iliyo na

maelekezo mazuri ambayo yanahitimisha shughuli zetu kwa mkutano huu tunaomaliza leo hii.

Waheshimiwa Wajumbe mashirikiano yenu ndio yaliyofanya kazi hii ikawa nyepesi na hatimaye leo kuikamilisha. Nichukue nafasi hii basi kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote lakini siachi kumshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wasaidizi wake ambaye amejitahidi sana kufanya kazi nzuri na kuwahudumia Wajumbe ipasavyo hadi kukamilisha shughuli zetu hizi.(*Makofi*).

Niwashukuru waandishi wetu wa habari, watu wa televisheni, wakalimali wetu lakini na wote wengine ambao walikuwa wanakuja kusikiliza shughuli zetu wakiwemo watendaji wa mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.(*Makofi*).

Wito umetolewa na Waheshimiwa Wajumbe kwamba wakati wa shughuli zetu basi watendaji wahudhurie ili kusikiliza kinachoendelea kwa ajili ya shughuli mbali mbali za serikali. Jambo ambalo ninadhani litasaidia sana katika kuwa pamoja katika kushughulika na kazi zetu kwa niaba ya wananchi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuakhirisha mkutano huu hadi tarehe 14 Mei, 2014 saa tatu za asubuhi barabara wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa niakhirishe mkutano huu hadi tarehe 14 Mei, 2014 saa tatu barabara za asubuhi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki**.**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

(Saa 1:45 jioni Baraza liliakhirishwa hadi

tarehe 14/05/2014 saa 3:00 asuhuhi)